

Hutoba Kutoka Katika Waebrania

Na

Andrew Connally

Yaliyomo

Hotuba Kutoka Katika Waebrania

MILANGO YA KITABU

Ufunuo Wa Mwisho	01
Mjumbe Wa Mwisho Na Malaika	03
Tutapataje Kupona Tusiposali	08
Kutimilika Kwa Huduma Ya Kristo	10
Ukuu Wake Kristo Kuliko Musa	12
Pumziko La Mkristo	14
Kuhani Mkuu Wa Mkristo	17
Kumsulibsha Kristo Mara Ya Pili	19
Kuuflkilia Ukamilifu	22
Tuamini - Nanga Ya Roho	24
Kristo - Kwa Mfano Wa Melkizedeki	25
Agano Bora Juu Ya Ahadi Bora	27
Mambo Ya1yo Takaswa	29
Dhabihu Ya Upatanisho	31
Saa Ya Kifo	33
Himizo Lililo Muhimu	35
Je! Ni Lazima Kuhudhuria Kanisani?	38
Hatumo Mionganii Mwao Wasitao	41
Imani Iokoayo	43
Pasipo Imani Haiwezekani Kumpendenza Mungu	45
"Pasipo" Tatu Kuu Za Waebrania	47
Kutia Unajisi Mambo Matakatifu	49
Mashindano Ya Mbio Zilizopo Mbele Yetu	51
Matatizo Ya Kurudi	53
Sinai Au Sayuni - Upi?	56
Wajibu Wa Mkristo	58
Kristo Asiyebadilika	60

UKURASA

Hotuba Kutoka Katika Waebrania

UFUNUO WA MWISHO

Waebr. 1:1-3.

Azimio: Ufunuo mkamilifu na wa mwisho wa Mungu unapatikana ndani ya Kristo na katika mafundisho Yake.

Shabaha: Kuonyesha kwamba Yesu Kristo na Agano Jipya ni ufunuo wa mwisho wa Mungu kwa mwanadamu.

Dibaji: Jifikirie kuwa u Myahudi aliyeishi kama miaka 1880 iliyopita, ikiwa ni mle Yerusalem au Palestina, chini ya kongwa 1a ugandamizaji wa Warumi. Tabia ya kuipenda nchi yao inaanza kuwaka mionganoni mwa ndugu wa Kiyahudi wanaofanya mipango ya kuasi. Kuna lalamiko la utukufu uliopita (historia yao), kuna lalamiko na kupendeza kwa ibada yao ya kale (sheria ya Musa), wanalo hekalu kubwa, ukuhani wa ajabu na sadaka za kuongoza mawazo yao na kuwageuze kutoka kwa Kristo. Yote haya waliyaepuka kwa ajili ya Kristo, sasa wengi wanaanza kuwa na mawazo ya pili (Second Guessing HS), wamejaribiwa kurudi nyuma. Kanisa lilikuwa likiudhiwa, haukuwemo sana utukufu wa mwili. Jaribu la kurudi nyuma lilikuwa na nguvu.

Mataifa hawakuwa katika hatari iliyo tofauti ya kurudia miungu yao; wengine wao bila shaka walirudia katika tabia na mazoezi yao ya zamani, lakini sio katika *miungu* ya washenzi; kwa Wayahudi ilikuwa tofauti, kwani Yehova alikuwa ni Mungu wa wakale na wapya pia.

Waraka huu kwa Waebrania ulikuwa wa kuonyesha kuwa la zamani limerithiwa na jipya, utukufu wa jipya ni mkuu kuliko utukufu wa la kale. Kwa hiyo, ombi la kuwa imara linafanywa katika msingi huu. Neno la ufunguo ni "bora" kusihii katika waraka mzima ni "kuwa imara."

Katika maneno yake ya kwanza mwandishi anakazia mambo mawili:

1. Upuzio wa maandiko, "Mungu amesema," waandishi wa Biblia hawatetei elimu ya upuzio, iIa tu wanadai mambo yaliyo ya hak'i.
2. Kujitegemea kunako ingiliana kwa ufunuo mbili. Mungu ni mwandishi wa yote mawili, hakuna upinzani, moja unategemea wenzie.

I. "Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu," 1: 1.

A. "Mungu ambaye zarnani," Agano la Kale limefahamika kama:

1. Kale: "Alisema na baba," ilikuwa ni miaka 400 tangu Agano la Kale lifungwe na Malaki; miaka 1500 tangu lianze. Lilitolewa katika uchang'a wa taifa, Kumb. 5: 1-3; Kuto. 34:27-28.

2. Lilifuatana na ahadi ya nchi kwa Ibrahimu, na kuwa na kazi mpaka uzao utakapokuja, Waga1. 3: 19.
 3. Halikukusudiwa kuwa la milele, Yer. 31: 31-34, na sasa linasemekana kuwa lilikuwa tayari kutoweka, Waehr. 8: 13.
- B. "Mungu - alisema - katika manabii," manabii walikuwa "wabashiri" wanenaji wa Mungu; alikuwa ni Mungu aliyesema ndani yao, "ndivyo asemavyo Yehova," "neno la Yehova," n.k. Waliifunua kweli ya Mungu, waliililia dhambi, wakimwonyesha Mungu, walitangaza mwisho wa mataifa, mwisho wa Israeli, na kuja kwake Masihi.
- C. "Mungu -- alisema - katika sehemu nyingi," kama walivyo litumia, ndivyo Mungu alivyolidhihirisha, "kanuni juu ya kanuni," Isa. 28: 10. Ndivyo ilivyokuwa kwa kidogo kidogo kwa zaidi ya miaka 1000 walikuwa na Sheria Waamuzi, Manabii, ndivyo ilivyokua na kuendelea.
- D. "Mungu - alisema - kwa njia nyingi," ilikuwa kwa namna nyingi. Ndoto, maono, sauti, malaika, aina, maneno ya manabii; ilikuwa ya kihistoria, kiuzima, amri, unabii, mithali katika yote Mungu alijidhihirisha Mwenyewe na mapenzi yake.

II. "Mungu mwisho wa siku hizi Amesema na sisi katika Mwana," 1:2.

- A. "Mungu mwisho wa siku hizi amesema," yaani, Mwisho wa kipindi cha Kiyahudi, Math. 17: 5; 2 Pet. 1: 3.
- B. "Mungu - amesema katika Mwana," ilikuwa ni "manabii wenye upuzio," Fidia ya "Mwana mtukufu," Kwani, neno lilikuwa mwili, Yoh. 1: 1-3; 1: 14; 1: 17-18; Mungu alikuwa ndani ya Kristo akidhihirisha na kupatanisha, 2 Wakor. 5: 18-21.
- C. "Mwana - mng'ao wa utukufu, chapa ya nafsi Yake," Mst. 3. Ufunuo mkamilifu na wa mwisho wa Mungu, Yoh. 14: 9. Yote jinsi Mungu alivyo, na yote aliyo nayo kwa ajili ya mwanadamu, Wakol. 2: 9-10; ukweli tupu ndani ya Yesu, Waef. 4:21; wokovu haumo katika mwengine awaye yote, Mdo. 4: 12. Mara moja tu imekabidhiwa, Yuda 3; ole wake yeche anayeongeza au kuondoa Kwake, Ufu. 22: 10-19.
- D. "Mwana - mng'ao wa utukufu," hayumo tena katika "sehemu nyingi, au njia nyingi" i1a wazi, Yoh. 16: 25; Rahisi, 2 Wakor. 3: 12; 11: 3; hakuna kivuli – bali kitu chenyewe. Hakuna tena ndoto, maono, au sauti, isipokuwa Kristo na Mitume Wake na Manabii. Hakuna nafasi ya Mohammed; Joseph Smith, Mary Baker Eddy au mwengineo! Wamekwisha!

III. "Mwana - Mng'ao wa Utukufu Wake," 1:3; Msemaji wa Mwisho.

- A. "Mwana," katika uhusiano Wake kwa Mungu:
1. "Mwana," kuonyesha uhusiano Wake kwa Baba, kwa hiyo, ni mkuu kuliko manabii na malaika. Uhusiano wa Milele.
 2. "Mng'ao wa utukufu Wake" - udhihirisho wa Mungu Mwenyewe. Hakuna mwengine anayeweza kufananishwa Naye!

3. "Chapa ya nafsi Yake," sehemu ya Mungu Mwenyewe, nakala halisi.
Hakuna anayeweza kuchapa wazi wazi kama hivyo.

B. "Aliufanya ulimwengu," Mst. 2. Muumba katika uhusiano wake na ulimwengu.

1. "Aliufanya ulimwengu," mwumba wa kila nyota, sayari, kila kizazi na kipindi, Wakol. 1: 15-18; Yoh. 1: 1-3.
2. "Akishikilia" - mhifadhi, kila kitu kimo mkononi mwake, kinachungwa, kinaongozwa, kinazuiwa, "kwa neno la nguvu Zake."
3. "Mrithi wa yote," Mst. 2. Mwenye kumiliki, sasa yote ni yake, Amepewa na Baba. *fn.* Zab. 24: 1.

C. "Amesema - katika Mwana." Katika uhusiano wake na ufalme, kanisa.

1. "Amesema - Mwana" Nabii wa Mungu, "Msemaji" Wake, Yoh. 6:38; 14:24; 12:49. *Neno* lake ni la mwisho. Kumb. 18: 15-19; Mdo. 3: 22-23; *fn.* "Hajanena kamwe mtu ye yote," Yoh. 7: 46.
2. "Utakaso wa dhambi," Kuhani. Agano Jipy lazima liwe na kuhani mpya na sadaka Hiyo sahihi. Alijitao Yeye Mwenyewe, Math. 20:28; Waebr. 9: 11-14.
3. "Aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu," Mfalme! Amezaliwa kuwa mfalme, Yoh. 18: 36-37!" Kuketi na kutawala," Zek. 6: 13; lakini aliinuliwa katika nafasi hiyo Alipofufuliwa kutoka katika wafu, Mdo. 2: 36-37. Kutafuta kumtawalisha katika kiti cha enzi cha Yerusalem ni kukataa Ufalme wake sasa!

Mwisho: Iwapo Yesu Kristo anadhihirisha Baba, kikamilifu, anatoa wokovu pekee, anauiahamisha ukweli wote na kulifanyia kanisa katika kazi yote njema, Wakol. 2: 10; Waef. 3: 20; 2 Tim. 3: 16-17, hakuwezi kuwa lingine la kufahamisha. Mungu hana ufunuo mwengine au mwenye kufunua mwengine. Sasa ni jambo la kumkubali Yesu kama nabii, kuhani, na Mfalme na kusimama imara, 1 Pet. 5: 12.

MJUMBE WA MWISHO NA MALAIKA.

Waebr. 1:4-14.

Azimio: Yesu Krista si mkuu kuliko "manabii" tu, bali ni mkuu kulika na malaika pia.

Shabaha: Kuonyesha ukuu wa Kristo kwa *malaika*, na *kwa* hiyo, neno lake lazima lionyeshe uimara.

Dibaji: Baada ya kuonyesha kuwa Mwana, mse maji wa mwisho, ni mkuu kuliko manabii, mwandishi sasa anahakikisha ukuu Wake kwa Malaika. Mwandishi anakusudia kuonyesha kuwa kama vile Mwana ni mkuu kuliko malaika, na hata hivyo neno la malaika laonyesha uimara lazima wote walishikilie neno la mwisho la Mungu alilolisema katika Mwana.

Kwa wengi wetu siku zote *Malaika* wamekuwa wa kufurahisha; makosa mengi yamefundishwa na waalimu wa uongo, ni jambo la kuburudisha kuijia Biblia kuona inenavyo juu ya soma hili.

I. "Malaika - Je, Hao Wote Si Roho Watumikao, Wakitumwa. Ku wahudumia Wale Watakorithi Wokovu," 1:14.

- A. Malaika ni watu walioumbwa, Zab. 148:2, 5; Wakol. 1:16.
- B. Ni watu wenye uwezo walio chini ya sheria ya Mungu, kama vile wengine walikosa, 2 Pet. 2: 4; Yuda 6, ambao mwisho wao ni kuteswa pamoja na ibilisi, Math. 25: 41; ambapo wengine wanamsujudia Kristo, Waebr. 1: 6.
- C. Malaika wametamani kuuona mpango wa madhumuni ya ukombozi wa Mungu, wakiwa na furaha nao, 1 Pet. 1: 12; Lk. 15: 4-10; lakini wamejifunza maendeleo yake kwa njia ya kanisa, Waef. 3: 10.
- D. Tangu mwanzo malaika wameyahudumia makusudi ya Mungu:
 1. Katika Agano la Kale, Ibrahimu na Lutu, Mwa. 10, 19; Ndoto ya Yakobo, Mwa. 28: 12; Musa pale Sinai, Mdo. 7: 53; Waga1. 3: 19; n.k.
 2. Kuhusu Yesu; Walitangaza kuzaliwa Kwake kwa Yusufu, Math. 1: 20; kwa Mariamu, Lk. 1: 25; Walishangilia kuzaliwa Kwake, Lk. 2: 13-14. Walimhudumia baada ya kujaribiwa Kwake, Math. 4: 11; Walimtia nguvu katika Gethsemani, Lk. 22: 43; Walilichunga kaburi na kutangaza kufufuka Kwake, Lk. 24: 1-6; Walimtambulisha kurudi tena kwa Yesu, Mdo. 1: 9-11; Waliipeleka roho ya Lazaro kuzimu, Lk. 16: 22.
 3. Kuhusu Mitume: Walisimama kando ya Paulo, Mdo. 27: 23; wataungana na Yesu wakati wa kurudi Kwake wakimsaidia kukusanya. nakuondoa *katika* Ufalme, Math. 13: 41-42.
 4. Leo ni wahudumiaji wa mkristo, Waebr. 1: 7; 1: 14.

II. Mwana Yesu, Mkuu Kuliko Malaika, 1:5.

A. Kwa Jina: "Amelirithi jina lililo tukufu zaidi," 1:4.

1. "Ndiwe Mwanangu," limerithiwa kutoka kwa waandishi wa Agano la Kale, Zab. 2: 7; Waebr. 1: 5; 2 Sam. 7: 14; Wana Wake ultangazwa na ufufuo wake, War. 1: 3-4.
2. "Kiti chako cha enzi, Mungu," 1: 8; imetangazwa hivyo kama Mungu na Mungu Mwenyewe, aliitwa Mungu kwa sababu alikuwa Mungu, Yoh. 1: 1; 1: 14.
3. "Wewe Bwana," 1: 10. Bwana kwa hiyo, Yehova, Zab. 102: 25; "Nilie" mkuu, fn. Kuto. 3: 14; ndivyo ilivyodaiwa na Yesu, Yoh. 8: 58 (Hakuna Mshahidi Wa Mungu anayeweza kufafanua namna hii!)

B. Kwa Mamlaka: "Kiti chako cha enzi, fimbo ya ufalme wako," 1: 8-9.

1. Mfalme, akitawala katika kiti Chake cha enzi, Waebr. 1 : 8-9; mistari yote miwili imetumiwa kumwonyesha Yeye akiwa Mfalme, kama Mwana, Ni Mfalme, Zab. 2: 1-6, 7; 2 Sam. 7: 11-14.
2. "Aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu," 1: 3. Ataketi na kumiliki mpaka maadui wote wamekuwa chini ya nyayo zake, 1: 13; atamiliki mpaka adui wa mwisho amebatilishwa, ambayo ni mauti, 1 Wakor. 15: 25-26.
3. Lakini anaketi katika kiti cha enzi cha Baba Yake, Ufu. 3: 21 na ataketi na kumiliki mpaka adui, mauti, ameangamizwa, na mauti itaangamizwa mwisho wa ulimwengu, Ufu. 20: 11-15; Yeye, kwa hiyo, yumo katika kiti cha enzi cha pekee anachotakiwa kukijaza!

C. Ni mkuu kwa nguvu za uumbaji:

1. "Aliufanya ulimwengu," 1: 2; Ni Mwumba, kwani ni wa milele, 1: 10-12. Vyote vimefanywa na Yeye, Wakol. 1: 16.
2. "Malaika wote wa Mungu wanamsujidia Yeye," 1 :7, kwa hiyo ni mwenye Ukuu, ambapo malaika wote ni wahudumiaji, 1: 7; 1: 14.
3. "Ni yeye yule jana, na leo na hata milele" 13:8. Habadiliki katika ulimwengu unao badilika, kwa hiyo, mtu anaweza kujenga juu yake kwa sasa na hata milele, Math. 7: 23-27.

III. Kwa Hiyo, Imetupasa Kuyaangalia Zaidi Hayo Aliyoyasema," 2:1--4.

- A. Haya ndiyo maneno ya ufunguzi wa kitabu kizima cha Waebrania.
- B. Ukuu na nguvu za Mwana zatuonya kuwa tuisitereze, kutojali au kurudi nyuma.
- C. "Kama maneno ya malaika yalikuwa imara tutapataje kupona tusipojaIi wokovu mkuu namna hii?"
- D. Hatuwezi! 10: 26-31; 10: 36-39; 12: 28-29.

Mwisho: Malaika ni viumbe vya ajabu vya Mungu, manabii wa kale walikuwa watu wa ajabu; lakini Mwana wa Mungu ni: Mwumba, Kuhani Mkuu; Nabii; Mfalme na Mtawala wa ulimwengu mzima. Katika mambo haya anastahili utumishi wa moyo ulio mkamilifu wa mwanadamu. Kumkataa Yeye ni kuangamia, kutereza ni kuishia katika maangamizi, kutojali ni kushindwa kabisa na daima, lakini kutii, 5: 8-9; ni uzima hasa. Nani atakayelikunja goti kwa Mfalme Yesu, akitubia dhambi na kumkiri na kubatizwa ndani Yake? Kwa nini Isiwe Sasa?

TUTAPATAJE KUPONA TUSIPOJALI?

Waehr. 2:3

Azimio: Mkristo asiyejali amekuwa zaidi kuliko kuwa "nje ya shughuli" - amepotea!

Shabaha: Kuonyesha jinsi wakristo wengine wasivyojali, kuonyesha dhambi ya kutojali, mwishoe kuonyesha matokeo ya kutojali.

Dibaji: Ukristo ni dini ya upendo, fn. Math. 22:37; 1 Yoh. 3:11; 3:14; Ni "njia Hiyo bora zaidi," 1 Wakor. 12:31; hata hivyo, hofu ina nafasi yake katika mafundisho ya Biblia na katika kuiffkia mioyo ya wanadamu, 2 Wakor. 5:11; Waehr. 10:31; 12:29; Yuda 22-23.

Hofu kuu inamngoja mtoto wa Mungu asiyekuwa mwaminifu kwa Kristo. Ni wakristo wachache sana ambao wamesaiwa juu ya ukristo. Watu huamini na kujizoeza na kitu iulani katika ulimwengu ambacho ni cha uongo na isipokuwa mmoja wapo akizishtusha "ninafikiri hivyo" zao na "ninaamini" zao na Neno 1a Mungu na mafikara yao ya manena, watakwenda *jebanamu* kwa furaha bila hata kujaH au kujali uthamani wa mambo ya kiroho.

Ukristo una maana zaidi kuliko kuhudhuria sala na kutoa, lakini ebu tuliangalie, na wengine wengi hawajajifunza hili bado! Kushindwa kuabudu mara kwa mara ni dhambi mbaya mno na kutasababisha mtu akapotea: Kwani, haujali wokovu mkuu.

I. Kutojali. Ibada Ni Dhambi Na Hao, Wanaojizoeza Kutojali Huku Watapotea!

- A. Kutojali ibada za siku zote ni kukosa kumtii Kristo, Waehr. 10: 23-31. Si "jambo linaoonekana kuwa linafaa," kama wengi wanavyoamini na kujizoeza! Linaonyesha tabia halisi juu ya vitu vya kiroho.
- B. Kunadhihirisha "namna ya utauwa," 2 Tim. 3: 5, lakini huwahadaa wenye hatia tu.
- C. Kutojali huko ni kikwazo kwa wengine, Math. 5:13-16.
- D. Ni kubaya mno kuliko ukafiri, fn. 2 Pet. 2: 20-22; na wote watakubali kuwa makafiri wote. wamepotea! Hili **nj** mbaya mno!

II. Kutojali Ibada Kunatuzuia Katika:

- A. Kushiriki Chakula Cha Bwana, kama anavyotuamuru Mungu kufanya katika siku ya Bwana, Mdo. 20:7; 1 Wakor. 11: 17-29. Kufanya jambo hili kuna sababisha usingizi wa kiroho - kifo!
- B. Kufundisha na kuonyana katika wimbo, Waef. 5: 19; Wako1. 3: 16. Hao wanaokataa kuimba, au wanaimba kama nusu wamelala ni wabaya vivyo hivyo!
- C. Kutoa katika vitu vyetu kama Mungu anavyoamuru, 1 Wakor. 16:1-2; 2 Wakor. 9:6-7. Kama ndugu walitota kama Mungu a1ivyowafanikisha wangefidia sadaka walizokosa kutoa, wasingekosa kutoa mara nydingi, Mal. 3:8.

III. Mkristo Asiyejali Ni Yule Asiye:

- A. Mweka Kristo na Ufalme kwanza, Math. 6: 33; wote wanahitaji kulitambua hili!
- B. Hawi dhabihu Hiyo hai, War. 12: 1 fn. Math. 16: 23-26.
- C. Mwenye kumwiga Kristo, 1 Pet. 2: 21.
- D. Fanya mvuto wake ufahamike kwa wema, Math. 5:14-16.

IV. Mkristo Asiyejali Lazima:

- A. Atubu au aangamie, Ufu. 3; 19-20.
- B. Akiri dhambi yake, 1 Y oh. 1: 9-10.
- C. Awe mwaminifu, Yoh. 14: 15; Lk. 6:46.
- D. Mungu hatakuachilia kutojali. Yer. 48:10.

V. Au Pengine Mkristo Asiyejali Atateswa Katika Sababu Hizi.

- A. Kinara cha taa yake kitaondolewa, Ufu. 2: 5. Ni jambo la kutisha lakini ni la kweli tupu!
- B. Atahukumiwa kwa mauti ya pili, Ufu. 2: 11.
- C. Jina lake litafutwa katika kitabu cha uzima, Ufu. 3: 5.
- D. Atapotelea jehanamu milele, Ufu. 20: 15; 20: 10.

Mwisho: Kwanini watu wapuuze wokovu wa milele wa roho zao kwa sababu ya kutojali? Ni laana juu ya mtu kwa wakati wa milele. Kuache kutojali kwako sasa, unawenza kushinda.

KUTIMILIIKA KWA HUDUMA YA KRISTO

Waibr. 2:5-8.

Azimio: Yesu Kristo alionja mauti kwa ajili ya kila mtu, Hi amrudishe mwanadamu katika mapendelezo ya Mungu.

Shabaha: Kuonyesha jinsi Yesu alivyoitimiza Huduma Yake ili amwokoemwanadamu.

Dibaji: Mawazo mawili makuu yako hapa, yamewekwa m bele za Waembrania kuyashikilia katika kweli, na kuwawezesha wasichukuliwe: Kwanza, enzi na kushindwa kwa mwanadamu; pili, kutimilika kwa kufanyika mtu na kudhihirishwa kwa Kristo.

Baada ya kuonyesha ukuu wa Kristo kuliko manabii na malaika, kisha kafikia mwisho kwamba yawabidi kulishikilia nena Lake, Paulo sasa anataka kuweka mbele zao kusudi la Mungu katika mauti iliyomdhihirisha Kristo msalabani.

Kristo alikuwa pamoja na Mungu, sawa na Mungu, kisha kama mwumba, lakini alijidhili, Wafil. 2: 5-8. Kwanini? Kwa kusudi gani? Ili akuze utukufu wake? Hata kidogo! Ila kwa ajili yetu sisi! fn. Yoh. 17: 5.

I. Utii - Enzi Na Kushindwa Kwa Mwanadamu, 2:5-9.

A. Uumbaji wa Mungu na kusudi lake kwa mwanadamu, 2: 5-9.

1. Mtu aliumbwa katika mfano wa Mungu, ila kidogo chini kuliko Uungu, Mwa. 1: 26-27; kama vile Mungu ni roho basi mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu wa kiroho, Yoh. 4:24; Waibr. 1:29; Mdo. 17:28.
2. Mungu alimfanya awe mtawala juu ya kazi za mikono yake aitawale nchi, 2: 7-8.
3. Mungu alimpa uhuru wa kuchagua, katika utii wake, Mwa. 2:15, ila sayari na anga Mungu anatawala, Waibr. 1:3.

B. Lakini mwanadamu aliufidhuli uhuru huo, akijifanya uhuru wake, hati ya dhambi, Mwa. 3: 4-6.

1. Kwa uasi akawa mwenye kupatwa na hatia badala ya kuwa mtawala wa milki yake, Mwa. 3: 16-19.
2. Mtu anaendelea kushikilia hati badala ya uhuru, akijiweka katika kongwa la utumwa wa dhambi, ambamo hawezi kujikomboa yeye mwenyewe, Wagal. 5: 1; 5: 13; 1 Pet. 2: 16.

C. Yesu alifanywa mdoko kuliko malaika, 2:9.

1. Mateso ya mauti: mwanadamu Yesu, kuteswa, kuona njaa, kuona kiu!
2. Amepewa utukufu na heshima; Yesu, Mfalme amepewa taji na kutukuzwa, Lk.24:46; 1 Pet. 1:20-21; Mdo.3:13.

II. Kusudi Takatifu Katika Kufanyika Mtu Kwa Yesu, 2:10-17.

A. Kumrejeza mwanadamukwa njia ya mateso Yak, 2:10-13.

1. Hili Iilitimilika kwa njia ya rnateso, kwani Kristo alifanywa mkamilifu

- kwa njia hiyo, Waebr. 5: 8; Lk. 13: 32.
2. Kanisa, mwili uliyorejezwa, ni udugu mkuu, ambao Yesu ndiye kaka mkubwa. Ni jamii ya Mungu, 1 Tim. 3: 15; Waef. 2: 19-20.
 3. Huu ni mwili uliopatanishwa, Waef. 2: 14-18; na kanisa ambalo litakabidhiwa kwa Mungu, Waef. 5: 25-27; kwa hiyo, hakuna wokovu nje yake!
- B. Kuiangamiza nguvu ya ibilisi, 2: 14-16.
1. Tangu Edeni ibilisi alikuwa ameshikilia uwezo juu ya mauti, Yesu alimshinda na kumfunga, Math. 12: 28-29; mauti haikuwa na nguvu juu Yake, 1 Wakor. 15:54-58; Mdo. 2: 23-24.
 2. Yesu sasa anazo funguo za mauti na kuzimu, Uiu. 1: 18; ambazo zitaangamizwa mwishoni, 1 Wakor. 15: 25-26; Ufu. 20: 14-15.
- C. Yesu anawaokoa hao wa Agano la Kale, 2: 14; Waebr. 9: 15; walioutafuta mji, Waebr. 11: 13; na pia hao wa Agano Jipy, 1 Wakor. 15: 20-25.
- D. Ili awe Kuhani Mkuu wa rehema na mwaminifu 2: 17. Kuhani Mkuu alifanya matoleo na maombezi kwa ajili ya watu, hili Yesu analifanya sasa, Waebr. 9: 11-14; 1 Yoh. 2: 1; Waebr. 7: 25.
- E. Kwa kuwa ni mtu, Anajua, anaelewa, na huguswa na kuona unyonge wetu, kwa hiyo twaweza kumkaribia wakati wa kuhitaji, Waebr. 4: 14-16.

III. Kwa Hiyo, Mwanadamu Hana Udhuru Kwa Kushindwa Kiroho.

- A. Myahudi hakuwa na udhuru kwa kuirudia torati, torati ilikuwa ni kivuli tu kikitambulisha kitu halisi, kitu hasa, Wakol. 2: 16-17. Mtu ana udhuru mdogo sana leo anaporudia mafundisho ya Kiyahudi!
- B. Mkristo hana udhuru kwa kuchukuliwa kutoka katika kuwaimara katia neno, na kuutoa uzima wake kwa kitu kinginecho, 2: 1-3.
- C. Mtoto wa Mungu hana udhuru kwa kujizoeza dhambi, kwa sababu katika ushindi Kristo anaweza kushinda majaribu, 1 Wakor. 12: 13. Dhambi za mtu zatokana na tamaa yake mwenyewe, Yak. 1: 13-15; kwa hiyo ausulibisha mwili pamoja na tamaa na shauku, Wagal. 2:20; 5:24.
- D. Mtoto wa Mungu anayeendelea katika dhambi hana udhuru kwani anamkataa Kuhani Mkuu Wake, 1 Yoh. 2: 1-2.
- E. Kila mkristo hana udhuru kwa kukosa kutimiza kitu fulani katika kanisa kwa ajili ya utukufu wa Mungu kwani Kristo alishinda na tumeambiwa, Wafil. 4:13; Waef. 3:20-21.

Mwisho: Mwanadamu aliumbwila ili atawale viumbe vyamungu; alipoteza haki hiya kwa njia ya dhambi. Kristo, kisha, akawa mtu ili amkomboe kwa njia ya dhabihu, kwayo akimshinda Shetani na nguvu zake; na akijiwezesha kuwa Kuhani Mkuu wa mwanadamu Hi mwanadamu awe na wakili pamoja na Baba. Je, utarejea kwa Mungu kwa njia ya Kristo?

UKUU WAKE KRISTO KULIKO MUSA

Waebr. 3:1-19

Azimio: Kristo ni mkuu kuliko Musa, kwa hiya, Iazima tumshikilie sana Kristo pamaja na nena Lake.

Shabaha: Kumfananisha Kristo na Musa na kuonyesha ukuu wa Kristo. Kwani hatuwezi kushindwa kuyaangalia maonya ya wa Israeli ambaa waliangamizwa jangwani.

Dibaji: Kristo sasa anafananishwa kama msemaji wa mwisho wa Mungu. Ni mkuu kulika Malaika wote, kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu. Ndani ya Kristo vitu vyote vinapatanishwa na Baba. Kujidhiri kwake Kristo kuna maana kwa jamii yote ya wanadamu.

Sasa Kristo anaonyeshwa kuwa mkuu kuliko Musa na tuanywe kwa mfano wa Waisraeli ambaao waliangamizwa jangwani.

I. "Mtafakarini Sana Mtume Na Kuhani Mkuu Wa Maungamo Yetu, Yesu." 3:1-2.

- A. "Mtume" - aliyetumwa kutoka kwa Mungu, mtume wa injili, Yoh. 20:21; War. 15:8. Fafanuzi ya Kristo.
- B. "Kuhani Mkuu," mmoja aliyefanya suluhu kwa dhambi za watu, Waebr. 2:17; 5:1; 5:10; 6:20; 7:26; 8:1; 8:3; 9: 11; 10:21.
- C. "Ndugu Watakatifu," wana, si watumwa. Wameletwa na Kristo, 2: 1.13. Fafanuzi ya wa Kristo.
- D. "Washiriki wa mwito wa mbinguni," si kiini tu, Lakini unapopata urahisi wake, utimilizo. 1 Wakor. 15: 24; Wafil. 3: 20.
- E. "Mtafakarini," kuona wazi wazi, kuelewa kikamiliifu, kutambua, wajibu kwa Kristo.
- F. "Maungamo yetu," ukweli, 2 Wakor. 9: 13; 1 Tim. 6:12-13; Waebr. 4:14; 10:23.

II. "Kwa Maana Kila Nyumba Imetengenezwa Na Mtu," 3:4-6. (Musa na Kristo Wafananishwa).

- A. Wote wawili "wamewekwa na Mungu," 3: 2. Maagano yote mawili yameteuliwa na Mungu.
- B. Wote wawili ni wa "nyumba" iyo hiyo, 3: 2. Mungu aliwaongoza wote wawili kwa watu wake.
- C. Kristo aliitengeneza nyumba, lakini "ilitengenezwa na Mungu," kwa hiyo Kristo ni Uungu, 3:3-4.
- D. "Musa, mtumishi katika nyumba, lakini ilitengenezwa na Mungu, kwa ushuhuda wa vitu vitakavyoonekana," 3: 5 fn. Hes. 12:7. Tafakari ukuu wa Musa: Kuzaliwa, kukua, elimu, kukimbia, kurudi, mapigo, kiongozi, mwenye kutoa sheria, n.k.
- E. Hata hivyo "Kristo kama Mwana," 3: 6. Yesu alikuwa zaidi ya mtumishi,

Mwana juu ya nyumba, moja ya kimwili; moja ya kiroho. Ufananisho kamili; hata hivyo kila mmoja alilitumikia kusudi 1a Mungu, 1akini Kristo ni Mkuu!

III. "Angalieni, Ndugu Zangu, Usiwe Katika Mmoja Wenu Moyo Mbou Wa Kutokuamini," 3:12.

- A. Mwisho wa kutisha wa hao wa 1iotoka Misri na hawakutii.
 - 1. Chini ya Musa walimchokoza Mungu na walanguka, 3:7-11.
 - 2. Na hata baada ya miaka Roho Mtakatifu alikutumia kushindwa kama onyo, Zab. 95:7-11.
- B. "Angalieni, Ndugu Zangu," 8:12, hatari hasa!
 - 1. "Sihi siku kwa siku." kwani dhambi ni danganyifu, 3: 13-15.
 - 2. Israeli aliquwa ni onyo kwa wote, "wasiotii," angalia Paulo ahoji kuwa "kutotii" ni "kutokuamini," 3: 12 na 3: 18-19.
 - 3. Mungu "alikuwa" na hana furaha na watoto Wake wanapokataa kusikia na kutii, 3: 16-19.
- C. Kama kwa hakika walivyoangamizwa watu milioni mbili katika jangwa, vivyo hivyo mifupa na makaburi yao yanaonyesha kuwa mtoto wa Mungu aweza kupotea! Hawakuingia katika raha yao, 4: 1 na sisi vivyo tusipotii, 4: 8-11.

Mwisho: 4:12, neno laweza kuyatambua mawazo ya moyo. Uwe macho! Vyote vi uchi mbele za Mungu. Mshikilie Kristo!

PUMZIKO LA MKRISTO

Waebr. 4:1-11

Azimio: Kunabakia, basi, raha kwa watoto waaminifu wa Mungu.

Shabaha: Kuonyesha raha atoayo Mungu sasa na hapo baadaye kwa ajili ya watoto wa Mungu.

Dibaji: Raha huleta kisomo mara kinachohusu waliochoka na kwa yeye ambaye mwili wake uliyoumia na maumivu na maradhi, au ambaye mwili wake umelemewa na taabu na uehovu wa miaka. Linakaribishwa na masikio hayo!

Kwa yeye aliyechoka na mizigo ya dhambi, na kutisha kwa adhabu yake, msemo wa raha katika Kristo lazima uamshe mishipa yake yote.

Tukisha shikilia kwa nguvu wazo 1a utu mwema na kubeba msalaba kwa ajiIi ya Kristo, lazima pawe na raha na tumaini ambalo hasa litayafunikiza, kumtia moyo mpitaji safarini mwake.

I. Iko Raha Ya Wakati Huu Kwa Mkristo.

A. Kila mmoja anayetikia mwaliko wa Yesu kuja Kwake, kupata raha sasa,

Math. 11: 28-29. Huwa mshiriki pamoja na Kristo, Waebr. 3:14; 3:6.

1. Raha kutakana na dhambi, na hofu ya matokeo yake, hupatikana katika raha na amani hii, Lk. 12: 4-7; War. 8:12.
2. Raha kutokana na fadhaa inayo waonea wengi, hupatikana ndani Yake na uangalizl Wake wa upendo, Math. 6: 25-34; Wafil. 4: 4-6.
3. Lakini kwa vile tumo katika mwili kuna uchovu, maumivu, maradhi, mateso na sononeko na huzuni vitakavyobebwa. Hivi hurahisishwa ndani Yake, Waebr. 13 : 5; 1 Pet. 5: 6-7.

B. Amani ya Kristo ni ya mkristo, Yoh. 14:27; kwa njia ya upatanisho kwa Mungu, Wako! 1: 19-22.

C. Furaha ya Kristo, katika utumishi wake, dhabihu Yake, na ushindi pamoja Naye, vivyo huwa ni mali yetu, Yoh. 15: 16; War. 14: 17; 1 Yoh. 5: 4.

II. Iko Raha Ya Baadaye Ambayo Hufanya Mateso Vote Kuwa Si Kitu, War. 8:18; 2 Wakor. 4:16; 5:7.

A. Raha ya Sabato huwangoja watu wa Mungu, Waebr. 4:9.10. Raha iliyobarikiwa kutokana na masumbuko na taabu, hili hutafutwa na Mkristo yote yakisha timilika, kwisha na kuachana na mambo ya sasa.

1 . Peponi: Kuna raha kabla ya mbinguni:

- a. Lazaro, kifuanini mwa Ibrahimu, na nguo zake kuu-kuu zimeondolewa, vidonda vimesahauliwa, alifarijika, Lk. 16: 25.
- b. Watakatifu katika raha, na joho nyeupe, wakingojea taji ya utukufu ya mwisho, Ufu. 6: 11; 14:13.

2. Mbinguni: Raha ya mwisho baada ya uzima na peponi.

a. Mbinguni na jinsi kulivyo:

- 1) Raha kutokana na uchungu; ambavyo hulemea na ku huzunisha maisha yetu. Chukizo katika biashara, katika watoto, katika rafiki wanaotusaliti; na hata katika sisi wenyewe tunapopungukiwa katika lengo na shabaha zetu.
- 2) Raha kutokana na ufukara; hao wasiojiweza kujipatia chakula, mavazi, dawa na mambo ya kufaa katika maisha, huko vitu vyote vitakuwa kwa wingi, fn. 1 Wakor. 3: 20-21; War. 8: 17.
- 3) Raha kutokana na huzuni za kuachana, machozi, kwa heri, vinavyoumiza mioyo - matengano tunapotakiwa nyumbani. Huzuni kubwa za matengano kwa njia ya kifo, huko, hakuna tena, Ufu. 21:4.
- 4) Raha kutokana na uovu na majaribu; ambavyo vime sumbuwa hapa, huko, vyote viko nje, Ufu. 21: 8; 22: 5.
- 5) Raha kutokana na maumivu ya mwiili; maumivu yanayotokana na vita vyta wakati wote - huko, mwili mpya, si uzee au unyonge, Wafil. 3:20-21.
- 6) Raha kutokana na makosa ya mafundisho ya uongo na uovu wa wanadamu yanayosumbua roho zetu! 2 Pet. 2:7-8.

III. Ushirika Na Shangwe Za Mungu, Kristo Na Watakatifu.

- A. Kuhusa jambo hili tunajua kidogo sana sasa, lakini Mungu atadumu kati ya waliokombolewa, Ufu. 21: 1-3; na sisi tutakuwa pamoja naye daima, Ufu. 7: 13-16.
- B. Tutamwona Yesu kama alivyo, 1 Yoh. 3:2, na tutakuwa Naye daima, 1 Wathes. 4: 17.
- C. Pamoja na wenge haki tutang'aa kama juu, Math. 13:43, na kumtumikia daima, Ufu. 22:3-5. Furaha ya kuwa pamoja na wenge haki wa vizazi vyote! Ufu. 5:9-14.
- D. Mungu Mwenyewe atayafuta machozi katika macho yetu, Ufu. 21: 4; na Yesu ataiondoa kiu yetu kwa maji kutokana katika chemichemi ya milele, Ufu. 21:6.

Mwisho: Hivyo ndivyo ilivyo raha. ya shangwe aliyolahidiwa mkristo, lakini sasa katika maisha lazima tufanye bidii kuingia katika raha hiyo, Waembr. 4:11.

Anapoangalia nyuma juu ya majaribu ya maisha katika shabaha ya ushindi, msalaba tuliochukua hautapunguka lo lote! Mizigo itasahauliwa; na tutashangaa jinsi tulivyoweza kujaribiwa na mambo ya dunia; utashangaa kwanini ulikataa toleo la Mungu kwa muda mrefu kama huo.

Je, hutaweza sasa, uanze katika barabara inayoongoza kwenye joho na taji, ile furaha na
raha inayowangojea waaminifu?

KUHANI MKUU WA MKRISTO

Waеbr. 4:14; 5:10

Azimio: Ukuhani wa Yesu Kristo ni ukuu kuliko wa Haruni katika Agano la Kale.

Shabaha: Kuonyesha kuwa mkristo an ahitaji ukuhani na kwamba Kristo ndiye Kuhani Mkuu na mkuu kuliko Haruni chini ya Agano la Kale.

Dibaji: Kazi iliyopo mbele ya mwandishi wa waraa wa Waеbrania, ni kumwokoa mkristo wa Kiebrania kutokana na upotofu. Anataka kulifanya jambo hili kwa kuonyesha ukuu, wa Kristo, wa agano mpya kwa lile la zamani katika vipengele vyake vyote.

Akishaonyesha ukuu wa Kristo kwa malaika kama Mwana; kama nabii kwa Musa, sasa anaendelea kuonyesha ukuuwake kama kuhani mkuu kwa Haruni.

Sehemu hii ya ukuhani wa Kristo na ukristo mara nyingi umedharauliwa, ukifikiriwa kuwa ni wa kizazi kingine kuliko chetu. Hili si kweli mkristo ni kuhani na atamhitaji kuhani mkuu kwa jinsi anavyotaka ondoleo la dhambi.

I. Maombi Na Faraja Za Kuwa Imara, 4:14-16.

- A. Faraja kutokana na ukuu na huduma ya Kristo, "Aliingia katika mbingu," 4:14.
 - 1. Mwana aliketi katika mkono wa kuume wa Mwenye Enzi, 1: 14.
 - 2. Anatangaza "yu hai siku zote," 7: 25.
 - 3. Ni Kuhani Mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, sasa mbele za Mungu katika Patakatifu, 9: 11-14.
- B. Faraja katika huruma za Kuhani Mkuu 4: 15.
 - 1. Mwandishi ameshalitaja hili, 2:17-18.
 - 2. "Udhafu" unyonge unaoharibu kustahimili majoribu kwetu, fn. War. 15:1. Yesu anajua, Yeye akiwa ni Mwana wa Adamu, alijaribiwa, hata hivvo bila dhambi! Anaelewa!
 - 3. "Alijaribiwa katika nafasi zote kama tulivyo," na Shetani; na Mafarisayo; na Masadukayo; na hata na Petro, Math. 16: 21. Lakini bila dhambi! Alishindana sisi tunaweza!
- C. Faraja kutokana na tunapokikaribia kitit cha neema, 4:16.
 - 1. Njia katika mahali patakatifu pa patakatifu ilitangazwa pazia lilipopasuka, wakati wa kufa kwake Kristo, Math. 27:51; njia imefanywakwa njia ya damu yake, Waеbr. 10:19-22.
 - 2. Kuna mahitaji ya rehema, neema na nguvu kilaa wakati za kusaidia, 1 Wakor. 10:12-13. Mkristo na aje na "ujasiri," hofu isiwemo katika kusema kwa ujasiri kwa ukunjufu, faraja. Kumbuka, Ufu. 21:8 (waoga).

II. Kuhani Mkuu Na Kutenda Kwake Katika Mambo Yanayomhusu Mungu, 5:1-3.

- A. Nabii alikuwa ni mmoja aliyesema na mwanadamu kwa niaba ya Mungu; kuhani mmoja anayesema kwa Mungu kwa niaba ya mwanadamu; aliteuliwa

- kutoa vipawa na dhabihu, 5:1.
- B. Kila kipindi katika vipindi vitatu vimekuwa na kuhani wake: Baba ndiye alikuwa nabii katika kipindi cha Mababu. Haruni na wanawe katika kipindi cha Musa; Yesu Kristo na kila mkristo katika kizazi cha ukristo.
 - C. Kipindi cha Musa kilikuwa na madoido; Haruni na wanawe walitakaswa, mavazi yenye madoido, kihema; vyombo vyake; dhabihu; makafara ya kila mwaka, n.k. Lakini vyote vilikuwa na udhaifu, zilihitajika dhabihui za nafsi, Waebr. 5: 2-3.
 - D. Pia ukuhani wa Agano 1a Kale ulipita na kipindi hicho, Waebr. 7:2.

III. Sifa Mbili Takatifu Kuhusu Ukuhani Mkuu, Zote Mbili Yesu Alikuwa Nazo, 5:4-6.

- A. Uteuzi Iazima uwe wa Mungu; sifa hii Kristo alikuwa nayo, 5: 4-6. Mungu alimteua Yeye kwa kiapo, Zab. 110: 4; baada ya nguvu ya uzima usiokwisha, Waebr. 7:16; 7: 28.
- B. Kwa kuwa Mungu alimteua kuhani mkuu kunaonyesha jinsi anavyohitaji watu wamtafute Yeye.
- C. Kuhani Mkuu Iazima awe na uwezo wa kuwa na huruma katika huzuni wenye kina; hili Kristo anaweza kulifanya, 5:7-9. Mtume anatumia jinsi Kristo alivyoona katika maisha kwa kuonyesha jambo hili, Lk. 22:39-46.
- D. Msingi wa kweli wa huruma umo, sio katika dhambi ya kawaida, 1akini katika mapigano na unyonge wa kawaida.
- E. Kwa hiyo, "Ndiye sababu ya wokovu kwa wote wanaomtii Yeye," 5: 8-9.

Mwisho: Kwa njia ya Yesu Kristo mkristo hutoa dhabihu zake kwa Mungu; kwa njia Yake huijia rehema na neema; kwa njia Yake anaweza kukikaribia kitu cha enzi cha Baba wakati wote.

Pamoja na ahadi hizi za ajabu na matoleo ya Mungu ndani ya Kristo wote waweza kushinda. Mfikirie Yeye, fikiria namna gano kwako, fikiria allavyotaka kukufanyia. Anao uwezo wa kukuokoa na yu tayari daima kuwaombea wote watakao kuja; kwanini isiwe sasa? Kwanini ungojee kitambo kidogo? Je, utakuja?

KUMSULIBISHA KRISTO MARA YA PILI

Waehr. 5:11; 6:8.

Azimio: Ulimwengu ulimsulibisha Kristo kwa mara ya kwanza, isipokuwa ni mtoto wa Mungu tu ndiye anamsulibisha Yeye mara ya pili.

Shabaha: Kuonyesha jinsi inavyowezekana kumsulibisha Kristo mara ya pili.

Dibaji: Wakati ndugu wanapojiruhusu wenyewe kulala kiroho wanamsulibisha Kristo tena. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kukubali kuwa ana hatia ya jambo hilo, wala ndugu wa Kiebrania, lakini wengine wao walikuwa na hatia ya jinaya iyo hiyo, na wengi katika kanisa wanayo hatia hiyo leo! Wakati wanaume na wanawake, walionunuliwa na damu ya Bwana wanapochoka na kuanza kuambatana na ulimwengu na kuridhika kiroho wamo katika msingi wa hatari.

Paulo aliwakemea Waebrania kwa ajili ya ujinga wao, wengine wetu wanahitaji kukemea huko leo! Ujinga ni dhambi, katika maisha ya mkristo nil. tukiutambua mapema na kuuacha, mapema sana tunaweza kurejezwu katika upende leo mtukufu; na tujifunze kemeo tukufu la Paulo na ombi na kuona kama dhamiri zetu zitatudunda, ikifanya inawezekana kuwa nil. hatia kama walivyofanya wakristo wa Kiebrania! Kwa hiyo uwe tayari kutubu!

I. Kimeo Tukufu: "Mmekuwa Wavivu Wa Kusikia," 5:11-14.

A. Fikiria umaana wa ufunuo, 6:11.

1. Kweli tunasemea urahisi wa injili, hata hivyo ina maana sana. Ni ufunuo wa mawazo ya Mungu, Hekima ya Mungu, War. 11:33.
2. Ukuhani wa Melkizedeki ni wa maandiko, mgumu kuusikia, 5: 6. Umetajwa mara mbili tu katika maandiko, Mwa. 14:17-20; Zab. 110:4; fn. pia na 2 Pet. 3: 16.

B. Hatua mbali mbali za maendeleo ya mkristo:

1. Watoto wachanga tukizaliwa katika jamii, lakini lazima tukue, 1 Pet. 1: 23; 2:2.
2. Mambo magumu hupatikana katika kukua, 1 Wakor. 3: 1-3; 14: 20.
3. Dalili za kukua, mtu anapoanza kuviacha vitu vya kitoto. 1 Wakor. 13:11; nguo, sanamu, msemo, n.k. Kua!
4. Kuwa watu wazima ndani ya Kristo, balehe, hili Mungu analitazamia, Yak. 1: 2-4; 2 Pet. 3: 18.
5. Hata hivyo wengine hubakia watoto wachanga au wenye kuugua kiroho; Kwa sababu ya: Kukosa chakula bora, 1 Pet. 2:2; Yak. 1:21; Yoh. 6:35; kukupasa kuacha, 1 Pet. 2: 1; Yak. 1: 21; 2 Tim. 2: 20-21; kukosa mazoezi, Waehr. 5:14; 1 Tim. 4:7-8; Yak. 1:22.

C. Sababu za upungufu wa maarifa baina ya wakristo: Sio kosa la Mungu! 2 Pet. 1:3.

1. Waebrania: moyo wao uligawanyika kati ya dini ya Kiyahudi na

Ukristo, kama mke wa Lutu anaanza kuangalia nyuma!

3. Wakristo leo: Miyo imegawanyika kati ya Mungu na mali, Math. 6:24; tunashughulika mno kuyawezesha mambo ya donia kuyasonga mambo merna, Math. 13:22. Kukosa kujisomea Biblia, "bila ujuzi" kutojali kufundisha, Kumb. 6:4-7; Waef. 6:4. Kutohudhuria ibada mara kwa mara, Waebr. 10:25; kuhubiri kusikojenga, kuhubiri kwa huzuni - hakuna kujisomea wa la dhabihu! Kutoyafahamu sawa maarifa, kutoka hotuba za kanuni za kwanza tu - hamna nyama! Upendo wa ulimwengu na ulivyo navyo ulimwengu, 1 Yoh. 2: 15-17.

II. Ombi Tukufu: "Tukiacha Kuyanena Mafundisho Ya Kwanza, Tukaze Mwendo Ili Tuufikilie Utimilifo," 6:1-4.

- A. Tukiacha mafundisho ya kwanza, "mkristo lazima aache kitu fulani, na kuendelea, "neno la mwanzo wa Kristo."
 1. Mkristo lazima akue kama mti unavyochipua katika mizizi, mtu kutokana na uchanga hukua na kujengwa kutokana na vitu vya kwanza.
 2. "Toba na imani." Toba kwa Mungu na imani kwa Kristo vilihubiriwa na Yohana Mbatizaji kwa Waebrania, Mdo. 19: 4; na Yesu, Mk. 1: 15; na Paulo, Mdo. 20: 21.
 3. "Ubatizo na kuwekea mikono," utakaso wa Kiyahudi; ubatizo wa Yohana, sasa vyote vimeachwa, pia kuwekea mikono kwa wenyewe kutoa dhabihu kwa Walawi, Lawi. 14.
 4. "Ufufuo na Hukumu," sehemu ya mafundisho ya awali, Mdo. 17:30-31.
- B. Tuufikilie utimilifu.
 1. Hakuna kituo, utimilifu ndio lengo, hali ya utu uzima, akili zaidi, fn. Wafil. 3:14-15.
 2. Mungu ameyawezesha maendeleo haya, Waef. 4: 13-14; Yak. 1 :25 "Sheria kamilifu iliyo ya uhuru."
 3. "Yu mkamilifu ndani yake yeye ambaye welekevu wa kibinadamu na kipawa kimepata maendeleo yanayolingana na matumizi, aliyoyatimiza makao ya mtu kwa kupata mfano wa Mungu, fn. Mwa. 1: 26; (Wescott).
 4. Mkamilifu katika kuuleta welekevu wote katika utii kwa Ukristo, 2 Wakor. 10: 3-5. Shughulika! Au utachelewa!

III. "Kwa Maana Hao Wailokwisha Kupewa Nuru, Na Wakaanguka, Haiwezekani Kuwafanya Upya Tena Hata Waka· tubu; Kwa Kuwa Wamsulibisha Mwana Wa Mungu Mara Ya Pili Kwa Nafsi Zao Na Kumfedhehi Kwa Dhamiri," 6:4-6.

- A. Hawa walikuwa wakristo wa kweli wakati moja: Hamna shaka na jambo hili!
 1. "Wakishapewa nuru" tia nuru, waliiona nuru, kuijua njia, Yoh. 1: 9; 2 Wakor. 4: 6.
 2. "Wamekionja kipawa cha mbinguni," nuru ya uzima iliyoletwa na Kristo, Yoh. 4: 10; 10:10.
 3. "Washiriki wa Roho Mtakatifu," Wagal. 4: 6-7; War. 8: 14-17; kipawa cha Mungu kwa watoto wake TU.
 4. "Wamelionja neno jema la Mungu," faraja, ahadi na tumaini.

5. "Nguvu za kizazi kijaeho," waliziona kazi za ishara za Roho Mtakatifu za kizazi eha mitume.
- B. "Kisha wakaanguka, haiwezekani kuwafanya upya tena."
 1. Wenye dhambi wengine waweza kurejezwa kwa Kristo, fn. Mdo. 8: 18-23. Wengine wameonywa kurejea kabla hawajaehilewa, War. 8: 12-14.
 2. Lakini wengine wanaweza kwenda mbali sana, warnekwenda mbali mno kuweza kuflkiwa na ye yote tena. Ndivyo hasa yanavyosema maneno katika ukurasa huu! Ohambi inaendelea na inaweza kutupeleka mbali sana ambako hatuwezi hata kutubu, kwa hiyo Mungu hawezikutusamehe.
- C. Ujinga ulimsulibisha Kristo wakati moja. Ulimwengu ulifanya hivyo. Na sasa ni ujingga, lakini ujinga katika moyo na maisha ya mkristo ndiyo njia pekee inayoweza kufanyika tena. Hao wanaopotoka humsulibisha Krista mara ya pili! Uko umbali gani katika barabara iendayo upotevuni?

Mwisho: Mwisho wa upotovu umeelezwa wazi katika Waebr. 10:26-31. Kama una wasi wasi na roho yako, unaweza kutubu, basi mshukuru Mungu hujaenda mbali namna hiyo. Usiichezee roho yako, tendo la pili kwa kutotii kwa hiari laweza kukusukumizia mbali sana ambako huwezi kuitwa tena. Rudi! Usichelewe kesho huenda ukawa umeehelewa mno!

KUUFIKILIA UKAMILIFU.

Waebr. 6:1-8.

Azimio: Mtoto wa Mungu ameonywa kuyaahya mafundisho ya kwanza na kuufikilia ukamilifu.

Shabaha: Kuonyesha wajibu wa mtoto wa Mungu kukua kuufikilia ukamilifu.

Dibaji: Kuna ulinganifu wa ajabu kati ya kuzaliwa, kukua na kuendelea kwa utu wa mwili na kiroho. Baada ya kuzaliwa na kuzaliwa katika ulimwengu, mtoto lazima akue mpaka anapofikia hatua ya mtu mzima, mwanarnume au mwanamke. Vivyo mtu wa kiroho huzaliwa kwa neno, akizaliwa katika jamii ya Mungu, ni mehang'a, ambaye ni lazima akue katika mambo ya kiroho kufikia mtu mzima ndani ya Kristo.

Katika maendeleo haya kuufikilia ukamilifu, kuna hatari ya kuanguka, kurudia katika maisha ya kale, ikiwa ni kwa ulimwengu au katika cheo cha kwanza cha dini. Mwandishi anaandika kuwaonya Waembrania kuhusu kuhitajika kwao kukua kuufikilia ukamilifu na hatari ya upotofu.

- I. "Kwa Sababu Hiyo, Tukiacha Kuyanena Mafundisho Ya Kwanza Ya Kristo," 6:1.
- A. Mafundisho ya kwanza ya Kristo: ukweli huo wa msingi yaliyofunzwa, katika mabadiliko kutoka dini ya Kiyahudi hadi Ukristo.
 - B. Hivi viachwe, sio kuvikataa, lakini viachwe kama mtu aachavyo msingi na kuendelea kulikamilisha jengo.
 - C. Mpaka hapa walishindwa kufanya jambo hili na walikemewa kwa ujinga wao na dhambi yao, 5:11-14.
 - D. Vitu vya kuachwa, 6:1-3, vitu vyote hivi lazima vieleweke katika mwanga wao mpya wa Ukristo, kuwa ni tofauti kutokana na matumizi yao ya kwanza chini ya sheria ya Kiyahudi.

- II. "Tuuufikilie Ukamilifu," 6: 1.
- A. "Endelea kukua kufikia utu uzima ndani ya Krista," kama 1 Wakor. 14:20; Waef. 4:11-16.
 - B. "Kwa watu wazima," waliobalehe, hao walia na sababu za kutumia aikiili zao kupambanua merna na mabaya, 5: 14. Neno sawa kama 6:1. (Kamilifu).
 - C. Kwa hiyo, ukamilifu ni utu uzima katika kupambanua mambo ya kimwili kwa kutumia werevu wa mwili. Namna anavyolitumia Mungu hufafanua maana yake.
 - D. Kwa "kuwakamilisha" watakatifu, Mungu ametayarisha:
 1. Sheria kamilifu (timilifu), Yak. 1:25.
 2. Waalimu na waangalizi waliohitimu, Waef. 4: 11-15.
 3. Matumizi ya majoribu, Yak. 1:2-4.
 - E. Upendo wa Mungu unahifadhi amri zake, 1 Yoh. 5: 3, upendo ambao

hukamilishwa na utii, 1 Yoh. 2:4-5.

F. Hili liwe ndiyo shabaha ya mkristo kila siku, ukamilifu katika kazi ya upambanuzi, kupambana na kujizoeza merna, Wafil. 1: 9-10.

III. "Maana Hao Waliokwisha Kupewa Nuru, Na Wakaanguka Haiwezekani Kuwafanya Upya Tena Hata Wakatubu," 6:6.

- A. Onyo: Hakuna anayesimama kimya. Ni kuendelea au kupotea na kupotoka. Ni kuendelea hata kuufikilia "ukamilifu" au kifo cha pole pole.
- B. Hawa waweza kuwa wakristo tu, 6:4·6.
- C. Mfano: Kama vile nchi itazaa mbegu au miiba na michokoo, kama pia maisha yatazaa kwa ajili ya Mungu na kubarikiwa au kuzaa maovu na kulaaniwa, 6:7-8.
- D. Basi, wote lazima waonywe, Wazazi na watoto wao, wazee na mikusanyiko; mtu binafsi na maisha yake. Ukikataa kukua na kujizoeza upambanuzi wa kiroho utakufa! Tafakari kucheza densi, kupapasana, mchanganyiko wa ku ogelea, n.k.
- E. Kupanda kote lazima kuwe na kuvuna kwake, sheria ya Mungu isiyo badilika, Wagal. 6:7-8; Waebr. 10:26-31.

Mwisho: Kama hujauacha ulimwengu kwa ajili ya Kristo, Je,! Hutafanya hivyo sasa? Kama hujayaacha mafundisho ya kwanza ya Kristo, Je! Hutaendelea kuufikilia ukamilifu? Kama unapigania kuendelea usife mayo, endelea kufanya kazi hiyo kwani ni baadae kabla hujafikiria, Waga1. 6:9-10.

TUMAINI - NANGA YA ROHO.
Waebr. 6:18-19.

Azimio: Tumaini ndilo nanga yetu ya roho, iliyo ya hakika na imara.

Shabaha: Kuonyesha tumaini tukufu la Mwana wa Mungu.

Dibaji: Tumaini hububujika daima katika mtu. Maisha yasiyo na tumaini ni maisha yasiyofaa kuishi. Watu wanaopoteza tumaini mara nyingi hufa kwa sababu hawataki kuishi tena.

Mkristo analo tumaini tukufu linaloshikilia roho yake wakati kimbunga na mabadiliko ya maisha yanapomonga kichwani. Mungu ndiye chanzo cha tumaini lote, War. 15:13.

I. Tumaini Limefafanuliwa Na Kuhakikishwa Kwa Mtoto Mwaminifu Wa Mungu.

A. Mungu Mwenyewe ndiye kimbilio letu la tumaini. Waebr. 6:18.

1. Mungu alimwumba mtu kwa tumaini, Zab. 16:19; 31: 24; 33:18; 38:15; 43:5; 71:5; 71:14; Yer. 17:7; Omb. 3:26. Tumaini hububujika daima katika roho ya mwanadamu.
2. Tumaini ni kutaka pamoja na kutazamia, Waebr. 11:6; War. 10:7; Mungu amesema, nimeamini, kwa hiyo nina tumaini! Zab. 119: 74.

B. Yesu Kristo ndiye tumaini letu. Tit. 2: 13; Waebr. 3: 6; 1 Pet. 1:3; 1: 13; 1: 21.

II. Tumaini La Injili Ni "Yesu Kristo Tumaini La Utukufu."

A. Kristo ndani yetu ni tumaini letu la utukufu, Wako. 1:27 na tumaini pekee alilo nalo Israeli, Mdo. 28:20.

- B. Tumaini ndilo msingi wa mwito wa injili, Waef. 1:18; 4:4.
- C. Katika tumaini tunaokolewa, Waeb. 5: 2-4; 8: 24;
- D. Katika tumaini tunaishi, 1 Wakor. 13: 13; War. 15: 13; 2 Wakor. 3: 12; Wafil. 1: 20; 1 Wathes. 1:3.
- E. Katika tumaini tunakufa, Wakol. 1:5; 1: 23; Tit. 3:7; Waebr. 6: 1; 1 Pet. 1:3.

III. Tumaini Letu Hutusukumiza - Kutupuzia Na Kuhifadhi: "Waliokimbilia Kushikilia Tumaini."

A. Hutupa kusema kwa ujasiri, Wafil. 1:20; 1 Pet. 3: 15.

B. Hutushikilia, Waebr. 6: 18-19.

C. Hututakasa, 1 Yoh. 3:3.

D. Hutufariji, War. 1:24.

E. Ni: "Njema," 2 Wathes. 2: 16; "limebarikiwa," Tit. 2: 13; "Li hai" 1 Pet. 1: 3; na "Bora," Waebr. 7: 19.

F. Hukamilisha silaha za mkristo, Waef. 6: 17; 1 Wathes. 5: 8.

Mwisho: Usiipoteze tumaini, kwani pasipo hiyo huna Mungu na Kristo, Waef. 2: 12. Na lishikilie roho yako kwa muda huu kwa wakati huo Iitatambulika katika milele!

KRISTO - KWA MFANO WA MELKIZEDEKI.

Waebr. 7:1-28

Azimio: Kristo ni kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki.

Shabaha: Kuonyesha kufanana kwa Kristo na Melkizedeki. DibaJi: Melkizedeki amefahamishwa katika sura ya 5:10. Hapa anazungumziwa kikamilifu zaidi. Mambo mengi mbali mbali ya elimu yanadumu kati ya wanafunzi kuhusu kipande hiki cha waraka. Wanaamini kuwa Melkizedeki anasimamia Kristo, Roho Mtakatifu au Malaika, au Henoko, Ayubu au wengine wengi.

Ni ujinga kufanya ukisio kuhusu neno la Mungu, kutokana na ambalo limesema Biblia tunaweza tu kusema kwamba Melkizedeki alikuwa mtu mwema, Mfalme wa Salemu na msimamizi anayetambulikana na kuhani wa Mungu, nchini mwake na wakati wake.

I. Mtu Wa Historia, Melkizedeki.

- A. Ibrahimu alijitenga na Lutu, akija kuishi katika Hebron, Mwa. 13: 18. Lutu alikuwa Sodoma. Sodoma ilivamiwa na wafalme wa Mashariki, wakiongozwa na Kedorlaoma. Lutu alikamatwa! Ibrahimu alimwokoa Lutu, akimshinda mfaIme kaskazini mwa Palestina karibu na Dani Lutu na watu walirudishwa majumbani mwao, Mwa. 14: 1-6.
- B. Melkizedeki, wakikutana na Ibrahimu akirudi, alitoa viburudisho, alimbariki na Ibrahimu alimpa cha kumi, Mwa. 14: 18.
- C. Haionyeshi kuwa Melkizedeki alikuwa na hulka nzuri zaidi kuliko za kibinadamu; ila tu alikuwa mtu mwema, mfalme wa kuhani.
- D. Melkizedeki: Mfalme wa haki; Salemu: Amani; kwa hiyo Mfalme wa haki, Mfalme wa amani, kuhani wa Mungu. Mfalme pekee wa aina yake asiye na aliye mrithi, bila mrithi wake katika nafasi yake kwa hiyo, hakuna kumbukumbu ya kizazi chake, kama Mwana wa Mungu katika mawazo haya, 1-3.
- E. Kama yeye, alikuwa mfano wa Mfalme wa baadaye na kuhani mkuu, Zab. 110: 1-4. Hili ndilo hasa aIloliona Paulo ndani yake.

II. Yesu Kristo, Mfalme Wa Haki, Mfalme Wa Amani, Na Kuhani Wa Mungu: Yaani Kuhani Mkuu Kwa Mfano Wa Melkizedeki.

- A. Waandishi wa Agano la Kale walimwona masihi kama:
 1. Mfalme, mpakwa mafuta wa Mungu, Zab. 45: 6-7.
 2. Mfalme na Kuhani, Zab. 110: 1-4; Waebr. 7: 3.
 3. Pamoja na amani akitawala katika Ufalme Wake, Isa. 9:6-7; 2:2-4.
 4. Kuhani na Mfalme, mshauri wa amani, Zak. 6: 12-13.
 5. Mfalme akisema kwa amani, Zak. 9: 9-10; Math. 21: 4-5.
- B. Waandishi wa Agano Jipywa wanamkubali Kristo kama:
 1. Mfalme wa Wafalme, Bwana wa Mabwana, Ufu. 17: 14.

2. Mfalme katika kiti cha enzi cha Daudi, Mdo. 2 :29-36.
 3. Kuhani Mkuu, Waebr. 4: 14; 5:5-6.
 4. Akiketi sasa, kwa hiyo, anatawala sawa na utabiri wa Zak. 6: 12-13; Waef. 1: 13; 1 :3.
 5. Anatawala sasa na kufanya hivyo mpaka mwisho wa dahari, 1 Wakor. 15:25.
 6. Anasema kwa amani, Waef. 2: 17.
- C. Kwa hiyo hao wanaomngojea Kristo kusimamisha Ufalme wa kidunia Yerusalem, kuketi katika kiti cha enzi cha Daudi na kutawala kwa miaka elfu moja wanangojea Bure!

III. Kwa Vile Yesu Kristo Amefanywa Kwa Miano wa Melkizedeki, Basi Ukuhani Wake Ni Mkuu Kuliko Wa Haruni, Unaowashawishi Waebrania Kurudia Katika Sheria.

- A. Kristo ni mkuu kuliko Haruni, kwa sababu kwa njia ya Ibrahimu Haruni alitoa ya kumi kwa Melkizedeki, 7: 4-10.
- B. Kristo ni mkuu kwa sababu Lutu alibarikiwa na Melkizedeki angali bado katika viuno vya Ibrahimu na mdogo huharibikiwa na mkubwa, 7: 6-7.
- C. Krista ni mkuu, kwa sababu alifanywa kuhani baada ya nguvu za maisha yasiyo na mwisho, 7:17.
- D. Kristo ni mkuu, kwa sababu Alichaguliwa kwa kiapo, 7:18-22.
- E. Kristo ni mkuu, kwa sababu Yeye ni Mwana, amekamilishwa daima, 7:26-28.

Mwisho: Swali kama hili laweza kuzuka, kwanini kufanya ufatanisho wenye madoido? Kwanini kutaka kuonyesha leo kuwa ukuhani wa Kristo ni kwa mfano wa Melkizedeki? Kuna haja gani kuonyesha kuwa sheria imepita? Kwanini mawazo yalemewe na jambo hili katika kizazi hiki?

1. Mwandishi anataka kuwaepusha na upotofu. Anasemezana pamoja nao, fn. Isa. 1:18. Watu siku zote hupenda sherehe na dhabihu na torati na mapokeo. Watu hujaribiwa na sheria hata leo: Shahidi: Kutoa cha kumi, muziki wa vinanda, ushirika wa watoto wachanga, uvumba, kuitunza Sabato, n.k.
2. Hili linawaonya pia wakristo hatari ya mapokeo; nguvu ya vitu vilivyo aminiwa kwa muda mrefu. Mungu baada ya kuandika Waebrania alituma Jeshi la Kirumi kuiharibu Yerusalem, hekalu na mambo yake yote ibada kusudi njia ya zamani isiendelezwe. Kuacha mapokeo ya kale ni vigumu, angalia Martin Luther, Wafanyakaji upya na Warudishaji wote walikuwa katika utumwa kwa makosa na mapokeo yao ya kale. Laweza kutokea kwetu leo!
3. Imani ya mkristo haikuja duniani kwa ghafula, lakini imeanza huko nyuma, katika agano la kale; kwa hiyo, ni muhimu, ila imekamilika ndani ya Kristo. Kama Mfalme wa Haki, Mfalme wa Amani Kuhani wa Mungu, Yesu anataka kutawala katika mioyo ya watu na kuwaombea mbele za Mungu. Je, utamruhusu ili akufanyie hivyo? Kwanini isiwe sasa?

AGANO BORA JUU YA AHADI BORA.

Waebr. 8:6-13

Azimio: Agano Jipywa ni bora kuliko Agano Ia Kale, kwa sababu liko juu ya ahadi zilizo bora.

Shabaha: Kuonyesha ukuu wa Agano Jipywa.

Dibaji: Kama vile ukuhani ulio bora umeteuliwa, bila shaka lazima pawe na sheria mpya, Waebr. 7: 12-13. Agano Jipywa hili ni kuu kwa lile la kale, kama ukuhani na dhabihu kwa lile la kale.

I. Agano Jipywa Ni Bora Kwa Sababu Halina Lawama Kwa Sababu Kuhani Wetu Hana Lawama, 9:1-7.

- A. Agano la kwanza lilikuwa na lawama katika mawazo ya uhusiano tu. Lilikuwa kamilifu kwa ambalo Mungu alilitolea; ila lilikuwa na lawama kwa sababu halikuweza kutoa njia ya msamaha wa dhambi, halikukamilisha lolote, Waebr. 7:19.
- B. Kwa njia ya Agano la Kale yalikuja maarifa ya dhambi, War. 3:20-21; 7:7; lakini haikuwa na dhabihu sahihi kwa ajili ya dhambi, Waebr. 10:1-4.
- C. Lilifanya kazi kama kiongozi kuwaleta Wayahudi kwa Kristo, Wagal. 3: 23. Lilikuwa la ahadi ya taifa-nchi iliyofanywa na Mungu kwa Ibrahim, Mwa. 12: 12; Wagal. 3: 19.
- D. Mpya lilikuwa kwa "uza" na "mataifa yote," ahadi ya kiroho, Mwa. 12: 3, kwa hiyo kuu zaidi. Ni ile "mpya" iliyotabiriwa na Yeremia, 31.

II. Agano Bora - Kwa Sababu Lilifanya Kazi Juu Ya Ahadi Bora, 9:6.

A. Kwa ndani na rohoni:

1. La kale Iiliwekwa katika kisafina cha mti wa Msita, mpya katika "mambo ya ndani;" la kale liliandikwa juu ya vibao vya mawe, mpya juu ya moyo. Lazima liele· weke, Math. 13: 15; Mdo. 8: 30.
2. Hufanya mawazo kuwa mapya, huumba upya, Waef. 4: 23; Wakol. 3:10.
3. Mungu lazima awe Mungu wao; ndani yake hupatikana mibaraka yote:
 - a. Kuwapo Kwake, Math. 28:20; 18:20; Wafil. 4:5.
 - b. Mwenye kutoa mibaraka ya kimwili, Math. 6: 33; Waebr. 13: 5.
 - c. Mwenye kuokoa kutokana na majaribu, Math. 6: 13; 1 Wakor. 10: 13.
 - d. Mahifadhi yake ya daima, 1 Pet. 5: 8; Mk. 10: 29.
 - e. Urithi wa milele, Waebr. 9:15; 1 Pet. 1: 3-5.

B. Mtu binafsi na mahali pote:

1. Chini ya la kale Myahudi alikuja katika uhusiano wa agano na Mungu kwa kuzaliwa kimwili na tohara; chini ya mpya kwa kuzaliwa upya na tohara ya moyo, Yoh. 3:3-5; 1 Wakor. 4:15; 1 Pet. 1:23; War. 2:18-29.

2. Chini ya la kale walizaliwa, halafu walifundishwa; chini ya mpya mtu lazima afundishwe kabla hajazidishwa, Yoh. 6: 44-45; Hili huondoa kabisa kabisa ushirika wa watota wachanga.
 3. Mungu ni Roho, Y oh. 4: 24; kwa hiyo, huduma ni ya kiroho, War. 12:1; ibada ya kiroho, Yoh. 4: 23-24; Wafil. 3: 3; maisha ya kiroho, Wagal. 5: 16. Hili hasa linahitaji kuzaliwa kiroho.
- C. Mwenye rehema na hutoa msamaha wa dhambi mkamilifu.
1. Matoleo na dhabihu chini ya la kale havikuweza kuondoa dhambi, lakini zilirudiwa kila mwaka wa upatanisho, Wala. 16. Hili liliweza kutakasa kutohana na unajisi wa mwili lakini sio dhamri, Waebr. 9:11-14.
 2. Sasa kwa damu ya Krista uko msamaha kamili wa kufuta kabisa dhambi, Mdo. 3:19; Waef. 1: 7; 1 Yoh. 1: 7; kwayo huongezwa kudumu kwa Roho Mtakatifu; Mdo. 2: 38; 1 Wakor. 6: 19-20; Wagal. 4: 6-7.

III. Agano Bora - Kwa Sababu Limewekwa **Wakf** (what?) Kwa Damu Ya Kristo.

- A. La kwanza liIiondolewa msalabani, Waef. 2:14; Wakol. 2:14; Waebr. 10: 9-10. Mpya litaendelea kwa muda wote na darnu ya Kristo idumuyo, Waebr. 13:20.
- B. La kale liliwekwa wakf kwa damu za wanyama. Mpya kwa damu ya Kristo, Waebr. 9:18-20; Math. 26: 28.
- C. Kama vile la kwanza lilipokea ujira wa haki kwa kuasi, Waebr. 2:1-2; pia la pili litakuwa na adhabu kali zaidi kwani agano hili ni kuu zaidi, Waebr. 10:26-31.

Mwisho: Ukuhani bora, agano bora, ahadi bora, dhabihu bora, nani aweza kulibadilisha? Nani asiyetaka kuitunza? Nani isipokuwa yule aliye duni ndiye ambaye hawezi kujali?

Ni katika agano tu ahadi. zinaburudiwa. Hutaingia katika agano hili pamoja na Mungu kwa njia ya kulikiri jina la Mwana Wake mbele za watu, ukizitubia dhambi zako, na kubatizwa katika mauti Yake. Katika tendo hili Ia utii unaifikia darnu ambamo agano limetiwa muhuri, kisha ahadi zinakuwa zako.

MAMBO YALIYO TAKASWA

Azimio: Vitu vyote ni vitakatifu chini ya Agano Jipy, vimefanywa hivyo kwa damu ya Kristo.

Shabaha: Kuonyesha utoaji wa yote mawili la kale na jipy, na kuonyesha ukuu wa lile jipy.

Dibaji: Tunakuja katika mazungumzo ya mpango wa 1a zamani na kuwekwa kwake wakf, na mpya na kuwek\la kwake wakf, kuonyesha katika kila njia ukuu wa mpya juu ya la kale.

Katika funzo hili maneno matatu yahitajika kueleweka:

1. Weka wakf: "Kuingiza, kutenga," Waebr. 9: 18; 10: 20, Thayer, Uk. 166.
2. Takasa: "Kutenga na mambo yasiyofaa na kuweka wakf kwa Mungu, tenga na kwa hiyo kufanya bila kuharibika," Thayer, Uk. 6.
3. Takatifu: "Kuweka kando kwa ajili ya Mungu, kuwa, kama kilivyokuwa, chake peke yake," Thayer, Uk. 7.

I. Patakatifu Pa Kale - Ni Miano Wa Papy, 9:1-10.

A. Kihema na vyombo vyake, 9:1-5.

1. Baraza la nje, mapazia, n.k. dhira 50 kwa 100.
2. Hema: Patakatifu, patakatifu pa patakatifu.
3. Vyombo: Kinara cha taa, meza, mkate wa onyesho, chetezo ya uvumba, sanduku la agano, kiti cha rehema, birika na madhabahu ya sadaka za kuteketezwa, fn. Kumb. 10:2-5; Hesa. 17:4,10; 1 Waf. 8:9.

B. Huduma ya kuhani, 9:6-8.

1. Sadaka zilikuwa kwa ajili ya dhambi, shukrani, amani na upatanisho wa kila mwaka.
2. Upatanisho wa kHa mwaka ndio ulikuwa dhabihu muhimu sana; ndani yake ilikuwa "wazitese" roho zao, ikionyesha toba. Hii ilikuwa aina ya sherehe za dini kwa namna yake, kwani haikuwemo toba, Taz. Wala. 16.
3. Vitu hivi vilikuwa kwa miano, 9:9-10. Yote haya yalikuwa ni kivuli tu cha vitu hasa vitakavyokuja hapo baadae, hema, ukuhani, torati n.k.

II. Dhabihu za Makafara Na Mbuzi Zalinganishwa Na Dhabihu Ya Kristo, 9:11-14.

A. Kumbukumbu Iimefanywa katika ndama kwa ajili ya sherehe za kutiwa najisi, na katika upatanisho wa kila mwaka kwa ajili ya dhambi, (Hesa. 19; Wala. 16).

B. Angalia mawazo yaliyofananishwa: Mnyama (mnyama aliye bubu), anaburutwa kwenda madhababuni, asijue kuwa damu yake inatolewa dhabihu kwa ajili ya hatia ya mwanadamu. Hata hivyo Kristo, kwa hiari, akijua, yote, hata hivyo bila dhambi, kwa kujiona kabisa na nguvu za utu wa milele anajitoa Yeye mwenywewe.

III. Kila Agano Limewekwa Wakf Au Kutiwa ldhini Kwa Damu, 9:15-22.

A. Kuwekwa wakf kwa la kwanza, 9: 18-21; Kuto. 24: 1-8.

1. Kitabu kilijaa na amri, ahadi na adhabu, vilivyotangazwa na Yehova, watu waliskia, walielewa na kuyakubali yote haya, waliingia katika agano na Yehova. Y ote mawili ya kinyunyizwa kwa damu.
2. Hema pia liliwekwa wakf kwa damu, lote likawa takatifu, likatakaswa (kuwekwa kando) kwa ajili ya Bwana, kwa hiyo, takatifu.
3. Adhabu kwa ajili ya kukufuru, kifo, Uzzia, 2 Mamb. 26; Uza, 2 Sam. 6; kifo pia kwa kutoa kisichofaa, Kora, Hesa. 16.

B. Kuwekwa wakf kwa agano la pili, Math. 26:28; Waebr. 9:16-17.

1. Kwa damu hii na njia ya agano hili wote' wanaoingia katika agano na Mungu huwa wametakaswa, Waebr. 10: 10; 13: 12; kwa hiyo, ni watakatifu, 1 Pet. 2:9-10.
2. Vitu vyote vinavyotakiwa na agano lazima vifikiriwe kuwa vitakatifu kwa sababu ya uhusiano huo kwa Mungu; mwili, maisha, huduma, ibada: sala, kuimba, kutoa, chakula cha Bwana, kuhubiri, vyote vimetakaswa na damu ya Kristo.
3. Vitu ambavyo havijatakaswa kwa damu ya agano lake havifai, ni najisi, kwa hiyo, havikubaliwi Naye, kwa mfano: Kunyunyiza, ubatizo wa watoto wachanga, muziki wa vinanda, mapokeo ya ibada za dini, majina ya madhehebu, kuadhimisha siku za kidini n.k. Hata kimojawapa kiliwekwa wakf na damu ya agano.

Mwisho: Chini ya Agano la Kale kuingiza kitu kisicho tukuzwa, kuasi amri iliyotukuzwa au mazoezi au kuasi amri tukufu, au kuingiza mtu wa kigeni, vyote vilileta kifo! Basi, mwisho wao utakuwaje hao wanaokufuru na kuvunja mipango ya Agano Jipy? Waebr. 10:28-29. Ni katika agano la Kristo peke yake.

DHABIHU NA UPATANISHO.

Waibr. 9:23; 10:18

Azimio: Dhabihu ya Yesu Kristo ni upatanisho kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.

Shabaha: Kuonyesha ni kitu gani kinachopatanisha kwa *ajili* ya dhambi za mwandamu.

Dibaji: Watu mara nyingi huanzisha makisio mengi kuhusu upatanisho, makisio ya watu mara nyingi hufanywa kuwa u~uzi. katika rnwanga wa neno la Mungu.

Shabaha kadhaa zinahitajika kuangaliwa:

1. Neno "upatanisho" linapatikana mara moja katika Agano Jipy, katika tafsiri ya Mfalme Yakobo (King James) katika Biblia ya Kiingereza, War. 5: 11. Neno limetafsiriwa "usuluhishi" katika tafsiri ya Kiamerika (American Standard Version).
2. Agano Jipy lamwonyesha Mungu akimtuma Kristo kufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. Watu lazima waikubali dhabihu hii kwa njia ya imani na utii kwa mafundisho ya Kristo.
3. Ni katika upatanisho ni: kuurudisha uhusiano, kati ya Mungu na mwanadamu, ambao ulivunjika kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.

I. Dhabihu Ya Yesu Kristo Inavyohusiana Na:

- A. Mungu - ni "usuluhisho." Sio kumkuliza Mungu, ila kurnhesabia haki Mungu katika huruma Yake kwa wanadamu wanaostabili kifo, War. 3:23-25; 1 Yoh. 2:12; 4:10; Waibr. 2:17; 9: 15.
- B. Dhambi - malipo - neno hili katika Agano Jipy limetafsiriwa tu: "Ondoleo" Math. 26:28; Mdo. 2: 38; "Kufuta" Mdo. 3: 19; "msamaha," Waef. 1: 7; "kutokumbuka tena," Waibr. 8: 12.
- C. Mwenye dhambi - ni "upatanisho," War. 5:11; 2 Wakor. 5:18-20; Taz. pia Waef. 2:16; Wakol. 1: 20-21.
- D. Mwenye kuokoa - ni "ukombozi," kufunguliwa na, kuachia kwa kulipa fidia, Waef. 1:7; Wakol. 1: 14; War. 3: 24; Waibr. 9: 15.
- E. Haya ni mambo ya kweli kama yalivyo katika maandiko, zaidi ya hapa tusijaribu kwenda! Tukubali: mtu amepotea katika dhambi, akihitaji dhabihu, ambayo ni Kristo, na kwa njia ya Kristo mtu hupatanishwa na Mungu, kwa hiyo Mungu huhesabiwa haki katika wema Wake, kwa ajili ya mtu, kwa sababu ya dhambi, anastahili kifo tu! Shukrani kwa Mungu kwa sababu ya rehema na upendo wa huruma usiosemekana na dhabihu ya Kristo isiyo na kifani!

II. Kukamilishwa Kwa Dhabihu Ya Kristo, 9:23-28.

- A. Kristo alikufa kama dhabihu kwa dhambi, 9: 26,28; Hakuna jambo la hamadi; ilikuwa kwa makusudi, kujidhiri Yeye mwenyewe kwa hiari na kikamilifu.
- B. Alipaa mbinguni kama kuhani, 9: 24.

1. Kuitakasa hemaya mbinguni kuifanya kitu cha haki ni Mungu ampokee mtu mwenye dhambi katika upendeleo wake na ushirika, 9:23.
 2. Kuonekana mbele za Mungu kwa niaba zetu, 9: 24.
- C. Atarudi tena kuja kutimiliza wokovu wa watu Wake, 9: 28, ukombozi wa miili yao, Yoh. 5:28-29.
- D. Angalia mkazo juu ya "mara moja". Kristo alikufa mara moja tu; alipaa mara moja tu; atarudi tena mara moja tu. Huu ni uihamisho mkuu kwa mpango wa huduma ya kila siku ya Haruni.

III. "Aondoa La Kwanza Ili Kusudi Alisimamishe La Pili," 9:9; 10:1-18.

- A. Mistari hii ni muhtasari wa hoja nzima mpaka hapa, Mst. 9 waonekana kama ufunguo wa ukurasa: "La kwanza" ukuhani, sheria, 7:12.
- B. Unyonge unaorithiwa kwa muhtasari, 10:1-4.
- C. Thamani ya dhabihu ya Kristo inayorithiwa, mara moja tu, 10:5-18.
- D. Hakuna haja ya kuitazamia nyingine, wala kwa Kristo kurudia ambalo amekwisha lifanya. Kazi imetimilika kama dhabihu inavyohusika.

Mwisho: Hili kwa ukamilifu linavunja dai la Wakatoliki kwamba Misa ni dhabihu; linaharibu dai la Wamamonni kwamba Joe Smith ni nabii na madai yao ya ukuhani; linaharibu dai la Waislamu kuwa Mohammed ni nabii, kwani angefunua kitu gani kwa ajili ya Mungu ambacho Kristo hajafunua tayari? Linawajibu wenyewe Utawala wa Miaka Elfu Moja, kwani hakuna lingine la kufuata kwa ajili ya dhambi za mwanadamu, au agano lingine au urudisho wa la kale.

Mwito ni kwamba "mpatanishwe na Mungu." Na kwa mkristo, "uwe mwaminifu."

SAA YA KIFO
Waebr. 9:27-28

Azimio: "Mtu amewekewa kufa mara moja."

Shabaha: Kuonyesha hulka za kifo na jinsi ya kufanya matayarisho sasa iji kukutana nacho.

Dibaji: Biblia si kitabu eha kifo, ila eha uzima, cha uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo. Lakini kinatuambia kuhusu kifo, hofu yake na ni kitu gani kinaehofuata kifo.

Hatupendi kufikiria kifo wala saa kitakapokuja. Kunakuwa na kujiona kama tunazama tunapojifikiria kwamba tunakaribia saa ya kifo, na ulio wa udongo, na uliokufa. Lakini ile saa yaja kwa kila mmoja wetu. Tunasikia mahubiri machache sana kuhusu saa ile. Biblia haisemi mengi kuhusu kifo kama isemavyo kuhusu hukumu itakayofuata.

I. Hulka Kadhaa Za Saa Ya Kifo.

- A. Kifo ni eha hakika, tukio Iinatokea kwa kila mmoja, Mhu. 9:2; 9: 5; Waebr. 9: 27. Kifo ni matokeo ya dhambi, Mwa. 2: 16·17; 3: 19; War. 5: 12; 1 Wakor. 15: 21.
- B. Kifo ni matengano, matengano ya mwili na roho, Yak. 2:26.
- C. Kifo hakina hakika wa wakati; kwani hakuna aliyekodi uzima kwa muda fulani, Mhu. 8: 8. Uzima ni mvuke, Yak. 1 : 24. Mambo yanayotizingira yanaonyesha kutokuwa na hakika wa saa ya kifo vizuri zaidi!
- D. Kifo huvunja vifungo vya dunia. Vifungo hivyo vinavyopendwa katika maisha huvunjwa katika saa ya kifo, huzuni, lakini huzuni zaidi mtoto wa Mungu anapokufa kiroho ambalo huvunja uhusiano wa jamii ya Mungu.
- E. Kifo ni cha upweke:
 - 1. Safari ya upweke, ya kifo hufanywa bila rafiki wa kidunia!
 - 2. Upweke wa Yesu bustanini, anapo jitayarisha kwa kito chake. Aliwachukua mitume kuwa pamoja naye, lakini walilala, Math. 26: 36-38.
 - 3. Upweke wa bustani na msalaba katika saa ya kifo, Lk. 22: 39-46; Math. 27:45-48.
 - 4. Upweke wa kutisha wa mtu anayeyaacha maisha haya pasipo Kristo, bali mkristo haendi peke yake, Waebr. 13: 3; malaika walimchukua Lazaro hadi kifuani mwa Ibrahimu, Lk. 16.
- F. Kifo hutia muhuri mwisho wa roho. Mwisho wa safari hutwiwa muhuri wakati wa kifo, fn. Lk. 16, katika uzima, tu, mtu anaweza kutubu na kuokolewa!

II. Basi Nini? Kitu Gani Kilichopo Mbele? Bali Tu Kuna Kuitazamia Hukumu Yenye Kutisha, 10:26-27.

- A. Biblia haionyi sana kuhusu saa ya kifo, kama inavyofanya kuhusu hukumu, jitayarische kukutana na Mungu! Arno. 4:12; Waebr. 10:31.
- B. Hukumu, Waebr. 9: 27.
 - 1. Kwa wote wenye haki na waovu siku ya kiama, Yoh. 5:28-29; Ufu. 20: 11-15; 2 Wakor. 5: 10.
 - 2. Hili litatukia wakati wa kuja kwa pili kwa Kristo, 2 Wathes. 1: 6-9.
 - 3. Kwa neno la Kristo vitabu vifunguliwapo, Y oh. 12: 48-49; Uiu. 20: 12.
- C. Umilele, wenywewe.
 - 1. Uzima wa milele umeahidiwa, na ndilo tumaini la mkristo, War. 6:23; Math. 25:46; Ufu. 2:7; 3:21.
 - 2. Ole ya milele kwa waovu, fikiria matengano kamili ya mema na maovu; tukiutumia umilele wetu na *mioyo* iliyogandana katika dhamiri, mateso ya fikara na kumuukumbu isiyokufa ya bahati tulizozikataa! Ni kutisha kwa aina gani huku!
- D. Milele pasipo na Mungu.
 - 1. Hamna urafiki jehanamu, yote haya yamekwisha.
 - 2. Hakuna watoto kule, wote wamo mbinguni, hakuna la kushangilia au kusaidia.
 - 3. Hamna kuimba, kusali, kulia na kusaga meno tu, Kile tu kinachoikamilisha ole, Ufu. 20:10, 15.

III. Nifanye Nini Ili Nikutane Na Kifo Kwa Tumaini Na Hakika?

- A. Mungu anawaamuru watu wote kutubu, Mdo. 17:30-31; Mdo. 2:38.
- B. Watubu na kurejea kwa Mungu, Mdo. 26: 19-20.
- C. Yesu anawaita watu wote kwake, ili wapate kupumzika, Math. 11: 28.
- D. Uwe mwaminifu katika mambo yote, Ufu. 2: 10.

Mwisho: Yesu Kristo kwa njia ya ufufuo ameutoa uchungu katika kifo, upweke na huzuni, 1 Wakor. 15:55-57; Waebr. 2:14-15. Huzuni hii huondolewa kwao wanaomkimbilia; waliooshwa na kutakaswa katika damu Yake.

Sasa, leo, wakati nafasi ipo, ikimbie għadhabu iliyowekwa kwa ajili ya waovu, Mungu anamkaribisha kila mmoja, nasi pia tunafanya vivyo.

HIMIZO LILIGO MUHIMU

Waefr. 10:19-31

Azimio: Kwa sababu ya milki ya mkristo ya sasa anawajibika kwa Mungu chini ya adhabu kali ikiwa atakataa.

Shabaha: Kuonyesha nini iliyo: milki yetu; wajibu wetu; na adhabu tukishindwa.

Dibaji: Akisha okolewa kwa dhabihu ya Kristo mtu huona furaha kuu - uzito wa dhambi hufanywa mwepesi, tumaini humpa upuzio mbele ya kikwazo cho chote, amani kuu na furaha hujaa moyoni. Kwa kitambo mapenzi ya dunia hypotea, ambapo mbingu na kuwa pamoja na Mungu na Kristo huonekana kwa utukufu.

Lakini mara nyingi muda unavyoendelea, anasa zinapoongezeka, au shughuli zinapomeza wakati wa mtu, maswali magumu yanapoanza au udhalimu au fedhuli inapoonekana, kuna hakika ya mapendeleo hayo ya kwanza kupoa na hatari ya kutojali; hatal'i ya kuchukuliwa katika uduni au kuurudia ulimwengu kunakuwa wazi kabisa.

Swali kisha huja, Ninawezaje kuitunza juhudhi na kuwa imara kwangu? Lazima nifanye nini kuilinda amani, tumaini, furaha, ambayo kwanza ilikuwa yangu? Hili ndilo swalii lilo mbele yetu katika sehemu hii ya waraka.

Mtu anaposoma kichwa cha somo hili, maneno mawili humchoma moyoni: "Kwa kuwa" na "Basi," yakionyesha tuliyo nayo na tunalowajibika kufanya na kila mmoja kufikia mwisho wa kuuhibadhi uimara ulio wa lazima katika wokovu.

I. "Basi, Ndugu, Kwa Kuwa," - Milki ya mkristo, 10:19-21.

A. "Kwa kuwa tuna ujasiri," 10:19, kumefafanuliwa kama "uhuru na uhakika usio na hofu, ushujaa mkunjufu." Ushirika usio na mashaka kwa Mungu, Waefr.

3:12; Waebr. 3:6; 4:16- Thayer.

1. Ujasiri huu sio wa majivuno, wala ukali, bali upole ule wa uthabiti usio tahayarika; ni utukufu ndani Yake, Mk. 8: 38; Ni ujasiri unaotokana na kuwa pamoja na Yesu, Mdo. 4:13.
2. Ujasiri machoni pa watu kuingia kwa Mungu kwa njia mpya na iliyo hai, iliyofunguliwa na Kristo na aliiifanya ifikiliwe kwa damu Yake. Yeye kama mtangulizi, amekwisha ingia, Waebr. 6:19-20.

B. "Kwa Kuwa na Kuhani Mkuu," 10: 21.

1. Mkuu kwa sababu Yeye ni Mwana wa Mungu, shabaha hii imehojiwa katika waraka mzima.
2. Mkuu kwa sababu amefanywa sawa na ndugu zake, 2:17-18; na kujaribiwa ila bila dhambi, 4:14-16.
3. Mkuu kwa sababu aishi milele, 7:25.

4. Mkuu kwa sababu dhabihu yake ni timilifu na kamilifu: Mungu, alisulibisha; dhambi, alilipa fidia, mwenye dhambi, alipatanishwa; mkristo alikombolewa!
- C. "Kwa kuwa tuna utakaso kamili," 10:22. Moyo umenyunyizwa kuacha dhamiri mbaya, mwili umeoshwa kwa maji safi Damu ile iliyio ya Kristo, Math. 26:28; Waebr. 9: 13-14; 1 Pet. 1:2. Kuosha, batizo, kuliko kwa njia ya mauti, War. 6: 3-4.

- II. "Na Tukaribie" - Masbarti Yakikua Kutohana Na Mambo Tuliyo Nay, 9:22-25.
- A. "Tumkaribie Mungu," 9:22. Hili ni la lazima kwa kuisbi kiaminifu; kuhifadhi juhudhi, amani na furaha lazima tukaribie. Yak. 4:8. Petro alifuata "kwa mbali kidogo," ndivyo wanavyofanya wakristo wengine. Petro alimkana Bwana na wewe utafanya vivyo!
 - B. "Wenye moyo wa kweli," waaminifu, fn. Yoh. 4:24. Kuwa imara katika waminifu.
 - C. "Na tulishike sana," ungamo la tumaini. Limo ungamwa mara moja, War. 10:9-10, sasa linaungamwa kila siku, Math. 10: 32. Tumaini hutegemea juu ya ahadi za Mungu; Mungu ni mwaminifu kutunza ahadi hizo, 2 Tim. 2:11-12.
 - D. "Tusiache kukusanyika pamoja," 10:25. "Sihi" "usiache." Hakuna mtu anayeweza kuishi *kiaminiiu mba/i* na ibada. Kubakia nyumbani na kusoma Biblia bakuchukui nafasi ya ibada pamoja na watakatifu! Basi, kukusanyika, mara nyingi kulimaanisha kifo cha mwili, na kutohudhuria kulimaanisha kifo cha kiroho; utalichagua lipi?

- III. "Maana kama Tukifanya Dhambi Kusudi" - Dhambi Kubwa, Upotofu, Na Mwisho Wake Wakutisha! 10:26-31.
- A. "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi," 10: 26. Je, dhambi zingine ni kubwa kuliko zingine? Kutohana na maandiko upotofu wa kusudi ni dhambi ambayo haiwezi kuwa na msamaha, 10:26-27. Huyu ni yule ambaye ame· kwenda mbali sana na haiwezekani kutubu na kurudi l Kupita tumaini lote.
 - B. "Mtu aliyeidharau sheria ya Musa," 10: 28. Mfano kutohana na Agano la Kale, 19:28; Kumb. 17:2-7. Ni ukubwa wa kiasi gani wa dhambi ya kumkataa Kristo, Mwana wa Mungu na damu Yake na agano Lake. Damu yake itakuwa moyoni au chini ya kisigino!
 - C. "Kupatiliza kisasi ni juu yangu, asema Bwana," 10:30. Mungu ni mwenye rehema, na pia ni mwenye haki na *anataka* utii, 12: 29.

Mwisho: Ni waaminifu kwa Kristo, unaohifadhiwa kwa kumkaribia Yeye, kushikilia sana, kuabudu, au ni upotofu ambaao utaishia katika maangamizi ya milele!

Na tuifikilie dhabihu aliyatufanya Kristo, fikiria kuwa mkristo kumekufaidia nini. Kisha na tutambue kuwa na yote ambayo Mungu ameyafanya, lazima tufanye mambo fulani kwa ajili yetu, ili kuutunza uhusiano huo pamoja na Baba. Waaminifu hadi mwishoni

ndilo tumaini pekee kwa uzima wa milele. Upotofu ni kuishia katika mwisho wa kutisha - kwanini usikimbilie katika tumaini hila sasa!

JE! NI LAZIMA KUHUDHURIA KANISA?

Waebr. 10:25.

Azimio: Njia za kukusanyika watakatifu zimeteuliwa na Mungu kwa ajili ya kukua kiroho, kukataa ni kutenda dhambi.

Shabaha: Kuonyesha kuwa kila huduma ya kanisa imewekwa kumleta mkristo katika kimo kikubwa zaidi cha utu uzima kiroho.

Dibaji: Waebr. 10:25 mara nyingi tumeitumia vibaya, imetumiwa vibaya inapowekwa kwa sala za Jumapili asubuhi TU! Jumapili hajatajwa hata kidogo. Kwamba inabusika na Jumapili hili Ii wazi kabisa, lakini kuiwekea kiwango katika sala moja ni kudharau kabisa maandiko yate na jinsi yanavyoelleza.

Sehemu kubwa ya washirika wetu ni wakristo wa JumapiIi tu. Ikiwapendeza hawahudhurii mafunzo ya mblia, ibada ya Jumapili asubuhi. Ibada za Jumapili jioni; ibada za Jumatano jioni; na kila mpango wa kazi uliowekwa ria wazee wetu. Wanatumikia nafasi, nafsi, ulimwengu na kwa nguvu hutangaza uhuru wao ndani ya Kristo!

Na tuangalie katika maandiko haya na kuona yanavyofundisha.

I. Wajibu Unahusika: "Msiache Kukusanyika," 10:25.

A. "Nyumba ya Mungu," Mst. 21, lazima tuikaribie, karibu na nini? Nani? Lini?
Haina maana hata kidogo kuhusu jengo, iHa mahali po pote ambapo watakatifu

WAMEKUSANYIKA KUMWABUDU MUNGU.

1. Huchukua "moyo wa kweli" - usio na unafiki. fn. Isa. 38:3.
2. Dhamana kamili ya imani, pasipo kutoamini, bila woga wa kukubali.
3. Kulisbikilia sana ungamo 1etu, bi1a kuyumba-yumba, Yak. 2:19.
4. Moyo umenyunyizwa kutokana na dhamiri mbovu, tn. 1 Pet. 3:20-21.

B. Ibada inatakiwa na kuwekwa na Mungu, Yoh. 4:23.

1. Hatari hasa tusipojali kuangamia kwetu, kwani tunaishi katika dunia mbili. Mathew Arnold amesema: "Lakini siku huleta vumbi lake, mara roho zetu zilizosongwa, kujazwa; na tunasahau kwa sababu tunalazimika na si kwa sababu tuna hiari."
2. Hii ni njia ya Mungu ya kutufanya tufungwe kwake, na kwa wenzi wetu, na jinsi gani tunakuhitaji!!

II. "Kuhimizana Katika Upendo Na Kazi Nzuri," 10:24.

A. Jambo lililo 1a lazima la Baba yetu ni kushirikiana na wenzi wetu, fn. Mdo. 2:22; 24:46; 2:47.

1. Ni mahitaji makuu kiasi gani leo, Waebr. 3: 13. Udanganyifu wa dhambi ndiyo nguvu ya majoribu. Jinsi majoribu yalivyo makuu zaidi ndivyo jinsi tunavyohitaji kuonyana. Kama tunazo nguvu za kutosha hatuhitaji

- nyama inayotolewa na huduma za wote kwani ni waehaehe sana wanaohusika katika mipango ya Kazi? Kazi ya binafsi, kutembelea; kutoa fn. Yud. 20!
2. TUMEAMRIWA! Tusiaehe kukusanyika - wazo la "Siku ya Bwana Tu" liko wapi? Kufanya hivyo ni kupoteza mafundisho ya ukurasa wote. Mamlaka ya sala zote inapatikana hapa.
 3. Wewe ni nani? Kipande eha Mungu, rnkristo katika upweke. Kitu gani kinaehokuwezesha kupata kuendelea kiroho? Upweke au ushirika? Nidhamu yetu inaegemea wapi?
 4. Lazima tuchochane na kuamshana katika maisha ya uungwana zaidi, Mst. 24. Mfano ni fafanuzi halisi! Askari aliyekuwa katika kufa alimwangalia Florence Nightingale na kusema, "Wewe ni Kristo kwangu."
 5. Lazima tutiane moyo. Wajibu wetu mkuu katika uzima ni kutiana moyo. Sheria ya Wanamaji yasomwa, "Hakuna ofisa atakaye zungumza kumkatisha tamaa ofisa mwenzake katika kutekeleza wajibu wake." fn. Ayu. 4: 4, tafsiri ya Moffat yasema, "Maneno yako yamewasimamisha watu juu ya miguu yao." Dunia yetu imejaa na wenye kukatisha tamaa na waliokata tamaa, tutafanya nini sisi tulio wakristo kuhusu jambo hili?
 6. Kwani wakati ni mchache! "Kwa kadiri mwonapo kuwa siku ile inakaribia." Huku ni kuja kwa pili. Ndugu amekaribia mno kwa miaka hii 1900, kuliko ilivyokuwa mtume alipoandika! Katika maisha yetu huenda tutakuwa tumechelewa, *in*. Math. 22: 14 (wengi wako baridi na wachache wameganda) fn. 2 Tim. 1:6.

III. Sababu Na Tokeo La "Kuacha Kukusanyika" 10:26-31.

A. Dhambi ya kusudi haiepukiki! Tunapojitenga, kutojali, kukataa, na daima kutafuta vya kadiri hilo hasa ndilo utakalovuna, 2 Wakor. 9:6. Kupanda au kuvuna ni Jipi hasa linalokuhusu? Unaweza kupanda kiasi gani au. "" kiasi gani unaweza kuvuna? Wagal. 6:7-8. Unapoteza ni wewe ndugu yangu! Usijitafutie kujihesabia haki, ila utakaso, linalokuhusu wewe ni lipi??

Msemo wa wakati huu unaonyesha dhambi ambayo mara kwa mara hushirikiwa, yn. hushirikiwa kwa kusudi. Kwa hiya hakuna tena dhabihu. Kwa hiyo neema yote ya baadaye na toba vimefungwa. Hawezi kutumainia msamaha tena. Dhabibi ya Krista yenye haina nguvu ya upatanisho tena. Ushindikano kamili wa kuweza kumrudisba *tena*. HaJj *yake* ya hatari ni toleo la kawaida la kosa lake la kusudi na pia adhabu ya haki inayotolewa na mkono Mtukufu. Sio kwamba anajifungia kutoka neema tu, bali pia mlango wa toba hufungwa nyumba *yake*; na mbele *yake* pana matazamio ya hukumu ambayo haiepukiki. fn. Mst. 27.

B. Kanisa la Agano Jipyä halikuweza kutangaza mambo mabaya ya imani *yake*! Watu wa aina hiyo ni upungufu mkubwa sana kwa kanisa. Washiriki wake lazima wawe na NIDHAMU au BURE. Upungufu wetu mkubwa zaidi ni maisha yasiyotosheleza ya watu wanaotabiri kuwa Wakristo!

C. Kutojali ni kukataa kabisa! Waebr. 2:4. Mkristo asiye tosheleza ALIKUWA na NI mtu anayeharibu hasa msingi wa kanisa.

D. Dhambi hii ya kusudi inajidhihirisha yenyewe katika karibu njia tatu:

1. Dhambi ni kumkanyagia Kristo chini ya miguu. Toleo la upendo haliwezi kuumia kwa uasi, uhuru au hatia ya kutanya dhambi. Jambo hilo hovunja moyo wa Kristo. Hadithi ya mtu aliyefungwa mateka na Hitler - aliishi, alijifunza kuwa mtoto wake alimpasha habari na kisha akafa. Kaisari alipambana na wauaji wake kwa dharau, mpaka alipouona mkono wa rafiki yake Bruto umeinuliwa juu yake - alijifunika kichwa chake na tandio na kufa. Tunaukataa upendo wa Kristo tunapotenda dhambi kwa kusudi.
2. Dhambi ni kushindwa kuona utakatifu wa vitu vitakatifu - (kuihesabu damu ya agano kuwa si kitu kitakatifu).
3. Dhambi ni kumkataa Roho Mtakatifu kudharau kabisa, utetezi, mwaliko na amri za roho na kwenda yako mwenyewe ni kumkana Roho na kuuhuzunisha moyo wa Mungu!

Mwisho: Katika yote haya msemo mmoja hutambulikana kwa urahisi - dhambi ni ya kuogofya, dhambi ni matokeo ya kujitenga pole pole na vito vya kiroho, Dhambi humhuzunisha Baba yetu; dhambi inatambulikana - twaweza kuiona ikitendeka. Kutojali na tabia mbovu htuondoa katika mambo ya kiroho. Hili haliwezi kuwa la Mungu, kwa hiyo, na tupiganie kuwa waaminifu katika kiJa sala. Na tujifunze kumpenda Mungu na kila mmoja na kuhimizana Siku ile inapokaribia.

"HATUMO MIONGONI MWAO WASITAO!"

Waеbr. 10:32-39

Azimio: "Hatuno mionganini mwao wasitao na kupotea, ila tuna imani ya kutuokoa roho zetu."

Shabaha: Kuonyesha kwanini sisi kama wakristo maca nyingi hukatishwa tamaa nil. kuwa baridi. Kazi yetu ya imani na bidii ya upendo huanza kupungua; *wakati mwingine* kama huu tunahitaji himizo na kutiwa nguvu kufanya "kazi za kwanza." Labda hakuna ukurasa mwingine unaofanya vema zaidi kama Waеbr. Sura ya 10-12.

Wakristo wa Kiebrania ambao wakati moja walikuwa wenye juhudhi, watumishi wenye kutoa dhabihu kwa Mungu walianza kupungukiwa nguvu· nil. walismama katika hatari ya kuzima imani, upotofu, "kuanguka kutoka *kwa* Mungu aliye hai." Taabu za udhalimu, matokeo ya dhambi katika maisha yao na uduni wa dini vinataka kuwaangamiza, nasi pia leo!

I. Kuna Haja Ya Mambo Waliyoyaona Katika Ukristo, "Zikumbukeni Siku Za Kwanza," 10:32-35.

- A. "Mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu," (*udbaImu* wa mwili) Mdo. 4:1-3; 4:21; 5:17-18; 5:38-40; 7:51-60; 8:1-4; 9:1-2; 12:14; 13:50; 14:5-6; 16:19, 24.
 - 1. "Mlipotezwa" - fn. 1 Wakor. 4: 9. Mliangaliwa.
 - 2. "Mashutumu" - kukemea, kusuta, kutupa katika meno; mafundisho ya upotofu ya Kiyahudi katika kuwatendea waliokuwa wakristo.
 - 3. "Dhiki" - kugandamiza pamoja, matokeo ya udhalimu.
 - 4. "Washiriki" - washiriki pamoja, 2 Pet. 1: 4.
- B. "Mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu," (kuharibikiwa na mali).
 - 1. "Kunyang'anywa" - kuharibu, wizi, kupokonya.
 - 2. "Furaha" - kupokea kwa upendeleo, fn. Yoh. 15: 20; Math. 5:10-12; 2 Tim. 3:12; fn. Mdo. 5:41.
- C. "Mlistahimili," Kwanini?
 - 1. "Mna mali iliyo njema zaidi" - Math. 6: 19-21; Lk. 12: 15.
 - 2. "Idumuyo" – 2 Wakor. 4:16-18; Yoh. 14:1-3; 1 Pet. 1: 4; Waеbr. 11: 16; 13:14; 11:10.

II. Haja Ya Kuwa Imara: "Basi Msiutupe Ujasiri Wenu: Maana Mnahitaji Saburi."

- A. "Mnabitaji ujasiri," kutokuwapo hofu, ambayo, hufuatana na uhuru wa kusema, uhakika, uwazi, hadhara, Y oh. 3:21; 2:28; 4:17; 1 Yoh. 5:14; Waеbr. 4:16.
- B. "Mnabitaji saburi," - kustahimili kiimara, Lk. 21: 19; 2 Wathes. 1:4; War. 5:3-4; Yak. 1:3; 5:7-11.

III. Hatimaye, Haja Ya Kanuni Ya Mkristo: "Hatumo Mio·ngoni Mwao Wasitao Kwani Mwenye Haki Aataishi Kwa Imani," 10:37-39.

- A. "Hatumo mionganini mwao wasitao na kupotea," - kurudi nyuma, kujitenga, fn. Mdo. 20:20, 27; (Ezek. 3: 18); Mk. 16:17-18; Mdo. 5:40-42.
- B. "Maana mwenye haki wangu ataishi kwa imani," fn. maisha ya imani yanavyoshuhudiwa katika: Waebr. 11:7; 11 24-26; 11:29-40.
- C. Kwa hiyo, na tuweke kando kilaa mzigo mzito na dhambi ile ituzingayo na Kukimbia! Waebr. 12:1-4.

Mwisho: Kama sio mkristo huwezi hata kuanza mbio! Kwanini usianze sasa kwa kuwa mkristo? Sisi tuliokwisha anza tunalazimika, 12:12-13. Mbingu zinangoja uamuzi Wako.

IMANI IOKOAYO

Waebr. 10:32-11:40

Azimio: Mungu ameielezea imani ile iokoayo kwa maisha ya Wenye haki wa Kale!

Shabaha: Kuonyesha maelezo ya Mungu ya imani iokoayo.

Dibaji: Mwanzo mzuri, katika kitu cho chote, ni kitu kizuri sana, ila isiwe ndiyo hati ya kufaulu na ushindi mwishoni; huchukua waminifu njia nzima katika ushindi wa kweli.

Waebrania walanza vizuri. Walifanya dhabihu kubwa, na walismama kando ya hao waliokuwa katika mateso. Sasa wanasmama katika hatari ya kusita. Walihitaji ujasiri na saburi ya kushikiilia. Haya na mahitaji ya kila mkristo katika kila kizazi.

I. Mwenye Haki Wangu Aataishi Kwa Imani, 10:38.

- A. Ni imani ile iokoayo. Kwamba rotu amehesabiwa haki kwa njia ya imani limekuwa ndilo fundisho lililotiliwa mkazo katika maagano yote, la kale na mpya, Haba. 2:4; imekaziwa Paulo, War. 1:16-17; Waga1. 3:11.
- B. Kwa mwaminifu kusita kila siku imekuwa ni kupata kutokuwa na furaha kwa Mungu - imetolewa kwa mfano katika historia ya Israeli, Waebr. 3; kwa mke wa Lutu, Lk. 17: 37; na imetiliwa mkazo na Yesu, Lk. 9: 62.
- C. Lakini Paulo anayo tumaini bora kwa hao anao waandikia; anaamini kuwa wanayo imani ya kuokoa roho, 10:39.

II. "Imani Iokoayo" Inaonyeshwa Katika Uthamani Wa Vipindi Vilivyopita.

- A. Habilii-na dhabihu yake, 11: 4, Habilii mchunga kondoo; Kaini mkulima. Tofauti ya wawili ambayo iliamua katika tabia ya Mungu ilikuwa ni imani ya kila mmoja. Ili mtu awe na imani inayofaa lazima ayasikie maneno ya Mungu, War. 10:17. Bila shaka Mungu aliwaambia la kutoa, ila Kaini hakutaka kusikia.
- B. Henoko - aliye enenda na Mungu, ambaye alichukuliwa na Mungu, 11: 5. Hii ni imani baina ya ulmwengu unaopatoka. Uovu ulikuwa ukikua haraka, Amo. 3:3.
- C. Nuhu - Aliyetii na kujenga mtumbwi katika kungojea gharika, ambayo haijawahi kuja wakati mwingineo. Hii ni imani baina ya ulmwengu unao dhihaki.
- D. Ibrahimu - aliyetii kuhama, akitafuta *kitu* ambacho Mungu aliahidi, 11:8-10. Hii ni imani baina ya ulmwengu wenye kuabudu sanamu.
- E. Musa - 11:24-26. Angalia akiwa katikati ya utajiri, ahadi ya nguvu, mwenye fahari ya utawala ita utu mwema, lakini "alichagua" kuteswa kwa ajili ya Mungu. Hii ni baina ya ulmwengu unaoshawishi.
- F. Licha ya hawa, wengine wote wenye thamani wa Agano la Kale ambao ni wengi mno kuweza kuwataja, 11:32-39.

III. "Kwa Kuwa Mungu Alikuwa Ametangulia Kutuwekea Sisi Kitu Kilicho Bora," 11:39-40.

- A. Kuna hasa pia sababu kubwa mno kwetu kuwa waaminifu katika ulimwengu uo huo. Hawa hawakuwa na ahadi iliyotimizwa kama tulivyo nayo; waliziona mbali au tokea mbali. 11 : 13; II: 39. Hakika tunayo bahati na kwa hiyo, udhuru mchache sana kwa kutokuwa waaminifu.
- B. Hawakukamilishwa pasipo sisi, 11:40. Wao na sisi tumekamilishwa ndani ya Kristo, 9:15.
- C. Kama wao na tujitahidi, 11:9-10; 11:13-16; 13:13-14.

Mwisho: Imani iokoayo ni imani yenyе utii; imani unayoshikilia hadi mwisho, bila kujali yanayotokea au magandamizi ambapo yaweza kuwekwa. Kusita ni kuangamia. Hakuna mabadiliko ila ni kuendelea mbele tu. Pamoja na waaminifu hawa wakishuhudia kuwa inawezekana, Mungu anatuhimiza kushikilia sana uhakika wetu kwa nguvu hadi mwisho.

"PASIPO IMANI HAIWEZEKANI KUMPENDEZA MUNGU"

Waebr. 11:1-6

Azimio: Kuna vitu ambavyo hatuna budi kuviamini ili tuokolewe.

Shabaha: Kuonyesha vitu vitatu vya kuamini ili tuokolewe.

Dibaji: Kitabu cha Waebrania ni kitabu cha imani. Hiki ni kizazi cha ukashaji. Watu wa sasa wamekataa kila jambo la msingi wa ukristo. Je, Mungu anaturuhusu kuamini tu kitu cho chote na kila kitu? Au Je, Biblia inaiundisha kuna vitu kadhaa ambavyo sina budi kuamini Hi niokolewe?

Katika somo letu tunajifunza namna imani ilivyo. Katika mstari wa kwanza na mstari wa ishirini na saba tunayo maelezo ya imani. Kwa kuwa imani yangu ndiyo nguzo au tumaini langu inafaa kujuu ninaloli amini.

I. Mmoja Lazima Aamini: "Kwamba Mungu Yuko Na Kwa mba Huwapa Thawabu Wale Wamtafutao," 11:6.

- A. "Mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yuko," (jinsi ya Mungu alivyo).
 - 1. Ushuhuda wote wa mtu unaonyesha kwa Mungu, War. 1:18-20. Mtu akiwa na mashaka juu ya ushuhuda wa macho yake mwenyewe, ameshapita msaada! Kuwa kama mtu asiyeamini kuwa Mungu yuko mtu lazima awe na mashaka juu ya ushuhuda woteanaouona, akikataa ushuhuda huo si mwaminifu.
 - 2. Nguvu na Uungu wa Mungu vyaoonekana kila wakati na mwanadamu kama vile majira yanayo badilika, Mdo. 14: 17.
- B. "Na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao," (ukarimu wa Mungu).
 - 1. Mungu hutunza kwa njia ya ufunuo wa maumbile, Mdo. 17:22-31; Zab. 19:1-6.
 - 2. Mungu hutunza kwa njia ya ufunuo wa maumbile ya juu sana, Yoh. 5:39-40; 6:44-45.

II. Mtu Lazima Aamini: Kwamba Yesu Ni Kristo, Mwana Wa Mungu.

- A. Yesu alilifanya dai hili Yeye mwenyewe, Yoh. 3:17-19; 8:24: (Yeye? Nani? Nini?)
- B. Katika ungamo tunalo jibu, Math. 16: 16-18; Wafil. 2:9-11; War. 10: 9-10. Kristo aliyefufuliwa, aliye hai.
- C. Imani hii si "kutokuona" hutegemeajuu ya ushuhuda, Yoh. 20:30-31. Ushuhuda halisi ni ufunuo wa Kristo, Yoh. 8:28; Math. 12:38-40; War. 1:3-4.
- D. Juu ya ufunuo Paulo anaweka shauri kwa ajili ya Kristo, 1 Wakor. 15:18-19.
- E. Kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu maana yake ni kukubali Mamlaka Yake na kuzitii amri zake. Si amini katika *ubatizo*, sala, *au* chakula cha Bwana,

lakini imani yangu imo katika Kristo anaye amuru na kutawala mambo haya mbali mbali. Imani ni katika Kristo – si katika tendo.

III. Mtu Aamini: Injili Kama Ufunuo Wa Haki Wa Mungu Katika Yesu Kristo.

- A. Katika injili imefunuliwa haki ya Mungu kwa mwanadamu, War. 1:16-17; hili lihubiriwe na kuaminiwa, Mk. 16:15-16.
- B. Injili imetangazwa kuwa ni leifo, kuzikwa, ufufuo na ushuhuda wake, katika 1 Wakor. 15: 1, 4, 11.
- C. Kwa hiyo, Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, 2 Wakor. 5:21; Waebr. 9:22; 10:4; Math. 26:28; War. 4:25.
- D. Alipoinuliwa akawa ni nguvu ya kuwavuta watu wote, mahali pote, Yoh. 12:32-33.
- E. Kwa hiyo, Anadai mamlaka yote, Math. 28:18; akitazamia imani, Yoh. 8:24; unataka toba, Lk. 13:3-5; anaamuru ubatizo, Mdo. 2:38; 10:48; namna ya mauti yake mwenyewe, kuzikwa na kufufuka, War. 6:17; 6:3-4; Yote ni matokeo ya imani, Wakol. 2:12.

Mwisho: Mambo muhimu kwa muhtasari; mambo haya. ni ya lazima katika wokovu. Huweka msingi wa tendo linalokubaliwa kwa Mungu. Kama unataka kumpendeza Mungu, basi kubali ukweli wa mambo haya, utii na kuwa na imani inayokubaliwa, ya kumpendeza Mungu machoni pake.

"P ASIPO" TATU KUU ZA WAEBRANIA.

Waebr. 11:6; 9:22; 12:14

Azimio: Wokovu wa mtu unaning'inia kwa kamba iliyo na "pasipo" tatu kuu zinazopatikana katika kitabu cha Waebrania.

Shabaha: Kuonyesha "pasipo" tatu na jinsi zinavyohusiana.

Dibaji: Kila mmoja anatambua kuwa kuna mambo mengi sana ambayo Biblia imeyaweka katika sehemu ya kukataa. Yaani, "Usi" au "Basi, yaondoeni." Hata hivyo iko sehemu ya kuk.ubalia katika ukristo, ikiwa ni sehemu Tukufu, ambayo Mungu ametutendea, au sehemu ya mwanadamu, ambayo lazima tujitendee sisi wenyewe.

Wokovu wa mwanadamu unaning'inia katika kamba iliyosukwa kwa nyuzi tatu za dhahabu. Nyuzi hizi ni "pasipo" tatu kuu za Waebrania. Somo.

I. Pasipo Imani Haiwezekani Kumpendeza - Mungu Lazima Aamini Kwamba Yeye Yuko
- Huwapa Thawabu Wamtafutao. Waebr. 11:6.

"Imani ni kusadiki kuwa Mungu anadumu nakwamba ndiye muumba na mtawala wa vitu vyote, mwenye kuwapatia na kutoa wokovu wa milele kwa nji, ya Kristo."

A. Amini kwamba Yeye yuko . . . " Imani katika kudumu kwa Mungu hakuwezi kubadiliwa na kitu kingineeho! Hakuna mtu anayekosa udhuru asiyetambua kuwapo kwa Mungu, Mdo. 14: 14-17; War. 1: 18-22. Pasipo imani hii mtu anakataa kuwapo kwake Mungu. Shida kubwa za kukana kuwako kwake Mungu.

1. Jambo ni la milele fn. 2 Wakor. 4: 18.
2. Uzima wa awali ulitokana na mambo yaliyokufa pasipo nguvu ya nje. fn. Mwa. 1:1.
3. Vitu vyote vinadumu has a kutohana na bahati inayoongozwa bila fahamu, Zab. 14: 1.

B. Huwapa thawabu wamtafutao.

1. "Mwenye kutuza" - "Mwenye kulipa ujira - anayelipa mshahara." Mdo. 17:27; Waebr. 10:35; 11:26.
2. "Kumtafuta Mungu" - Mungu hajatuza imani ya mtu mpaka imani hiyo inapojionyesha yenyewe katika njia fulani, inayodhihirika kwa nje! Imani isiyotenda imekufa, Yak. 2: 26. Tunamtafuta Mungu kwa imani, na imani hiyo hutuzwa inapomtii Mungu, fn. Mdo. 15: 9; I Pet. 1: 22; Wagal. 5: 6.

II. "Pasipo Kumwaga Damu Rakuna Ondoleo, 9:22.

- A. Ushuhuda wa kutosha katika ukweli huu, Math. 26:28; Mdo. 20:28; War. 3:24-25; Waef. 1:7; 2:13; I Pet. 1:18; Ufu. 1:5; 7:13-14; 1 Yoh. 1:7.
 - B. Katika kila kizazi Mungu amewataka watu kukaribiana nadamu, Mwa. 4:3-5; Kuto. 12:21-23; Waebr. 9:21-22; 9: 19-20; 9:11-18.
 - C. Sina ujuzi wala' filosofia kuhusu upatanisho. Kwanini Mungu alichagua "damu" sijui, kwamba aliichagua ninajua.
- III. "Pasipo Amani Na Utakatifu Hapana Mtu Atakayemwona Mungu," 12:14.
- A. "Amani" - amani kati ya mtu na mtu, kulingana, kufanana," War. 14:19; 1 Pet. 3:11; Yak. 3:18; Waef. 2:14-17; Math. 5:9.
 - B. "Utakatifu" - (utakaso) War. 6:19-22; 1 Wathes. 4:3; 4:7; 2 Wathes. 2:13.
 - C. Tunawiwa kwa ajiIi ya utakatifu kwa Kristo, 1 Wakor. 1:30-31.

Mwisho: Kwa kuwa "pasipo" hizi tatu ni za lazirna kwa wokovu wetu, si vigumu kuona uhusiano uliopo kati yao.

Imani

Amani na Utakatifu



“Ubatizo”

Damu

“Upya ya Uzima.”

War. 6:3-4

“Kifo”

Waef. 2:8-10

KUTIA UNAJISI MAMBO MATAKATIFU

Waebr. 12:14-17

Azimio: Mtoto wa Mungu lazima awe mwangalifu asije akatia unajisi mambo Matakatifu, kwani hili limekatazwa! Kuna sehemu za hakika ambapo tunatia unajisi.

Shababa: Bila kuwa na mawazo kunatuongoza katika kutia unajisi mambo matakatifu ya Mungu, basi, tuonywe kuwa macho!

Dibaji:

1. Esau anaweza kuwa mfano mzuri sana ni matokeo gani makali yanayoweza kuja kwa kushindwa kushukuru kwa ajili ya mambo matakatifu ya Mungu; Makosa mengi huanzia katika, "sikufikiria."
2. Unajisi mara nyingi umefikiriwa kuwa kama "kutukana" kuliko wazi, lakini mara nyingi huwa na maana zaidi kuliko hivyo. Tusi ni ufahamisho wa nje wa unajisi. Unajisi ni hali ya nia, moyo na maisha - kuapa ni ufahamisho wa nje tu. Unaweza ukaacha "kutukana" pasipo kugusa moyo wala hali ya kweli. Ufikie katika moyo na utabadilika kila wakati.
3. Unajisi: fafanuzi - "Ya kwanza, kuruhusu kukanyagwa, kufikika, kiwanja cha kupuria, kwa hiyo kisicho kitukufu, kinyume cha utaatifu kinachokosa uhusiano wote au udugu kwa Mungu," fn. Waebr. 12: 16.

I. Mahimizo Na Maonyo Kujikinga Na Unajisi - Mst 14-15.

A. Kutafuta "amani," "umoja - upatano."

1. Mkristo amefanya amani yake na Mungu, War. 5:1; 5:11.
2. Katika amani na wakristo wenzie, 1 Wathes. 5: 13.
3. Ana amani moyoni mwake, Wakol. 3: 15.
4. Kutafuta kuwa na amani na watu wote, War. 12: 18; Mst. 14 MIFANO.

B. Kutafuta "utakatifu" utakaso wa moyo na maisha.

1. Amefanywa katika utakatifu, Waef. 4:24: 1 Wakor. 1:1-2.
2. Hadi kufikia utakatifu kamili, 2 Wakor. 7:1.

3. Kuutafuta, Mungu alivyo mtakatjfu, 1 Pet. 1: 13-17.

- C. "Pasipo huo hakuna atakayemwona Mungu," "Milango ya mbinguni hufungwa kwake anaye ingia katika hali ya DHAMBI" fn. Ufu. 22: 14-15.

II. Maonyo Juu Ya Unajisi - Mst. 15.

- A. "Ye yote akipungukiwa," si kujiangalia sisi wenyewe tu lakini kila mmoja kwa mahitaji ya ndugu yake, Wagal. 6:1-2; Waebr. 3:12-14; 10:24.
- B. "Shina la uchungu," fn. Kumb. 29: 18, "Lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga" - MIFANO.
- C. "Mwasherati" - 1 Wakor. 6:13; 6:18, 19, 20, Mst. 13, 14, 15. (Ni KAHABA KWAKO !) Afanyaye uasherati ni NAJISI.
- D. "Asiyemcha Mungu" kama Esau. Aliyeuza urithi wake lile ambalo ni takatifu. ukuu na mamlaka na pia na uzazi wa Masihi. Kutojali sana wa mzaliwa wa kwanza - kipande maradufu, baraka kuu, Mungu na damu Yake na aganao lake. Damu yake itakuwa...

III. UFAHAMISHO WA UNAJISI LEO.

- A. Uungu -- Jina la Mungu, linalo msimamia - Yeye Mwenyewe! Vyote ambavyo alivyo navyo, Zab. 111:9; Wafil. 2:9-11 - hunajisiwa kwa "kuapa" hasira. ghadhabu, n.k. Mizaha - Ad Nansau.
- B. Kanisa - Hekalu la Mungu, 1 Wakor. 3: 9; 3: 16-17. Mwili wa Kristo, Waef. 5: 23-27; makazi ya Mungu katika Roho - Waebr. 5:19-22. Hunajisiwa kwa kuliananisha na kilabu, nyumba ya wageni, kudharau huduma zake za ibada, kazi, - au "kufanya biashara."
- C. Nyumba na ndoa - ilianzishwa na Mungu - chungu mzima cha kufanya maisha nyumba maskani! Naamu na upendo chungu mzima wa kufanya kuishi pamoja katika NDOA! Zinaa inayokubaliwa - mwanaume na mke wa kwanza! Bila upendo - ni *kuishi* kama wapangaji tu! Uhusiano huu ultakaswa na Kristo, Waebr. 13:14, unatawaliwa na Mungu, Math. 19:6. (Mifano Madalene) unajisi wa daima - mke anayeshikilia ashiki juu ya kichwa cha mume kama upanga wa Damocles! Majaribu ya watu wa umri wa kati! Wazee hukua katika kutokujali kufundisha!
- D. "Urafiki" fn. Math. 11: 19 inaonyesha mtu tunayempenda, mpenzi, ninajiona sana katika jambo hili nimepotea na rafiki au wawili katika maisha yangu-ukinajisi uhusiano huu umeharibu umoja mtukufu! Tunajua mengi - tu marafiki wa WACHACHE sana!

Mwisho: Kipimo kitukufu cha haki Ya Mungu hudharauliwa, uhuru wa mtu humfanya kutenda dhambi! Kukosa kutunza humaanisha upotevu wa ushawishi - kutoangalia vifungo vitakatifu.

MASHINDANO YA MBIO ZILIZOPO MBELE YETU

Waebr. 12:1-3

Azimio: Mkristo Jazima akimbie na saburi mbio zilizopo mbele zake.

Shabaha: Kuzungumzia mbio zilizopo mbelc ya mkristo na kututia nguvu sisi sote kufanya kila kitu kinachotakiwa kuzimaliza mbio hizo.

Dibaji: Kila mtato wa Mungu huchoka na mapigano yake na nafsi, Shetani na dhambi. Sisi, basi, tumo katika hatari ya kudhoofu na kulegea katika mbio za mkristo.

Waebmania sasa wamekwisha ifikia sehemu hiyo katika maisha. Walikuwa katika hatari ya kusita, 2:1-4; walihitajika kunoa kusikia kuliko kuwa butu, 5:12-14; walihitajika kushikilia saburi, 10:32-36; walihitajika kuweka kando mzigo mzito na dhambi na kuzikimbia mbio zilizopo mbele yao, 12:1-3.

I. Muhtasari Wa Mbio Za Imani, 12:1-4.

- A. Mbio za mkristo ni "mapigano na dhambi," 12:4. Ni mapigano magumu, *in. Lk. 13:24.*
- B. Inawezekana "hata kumwaga damu," 12:4. Kujikana, kubeba msalaba ni nishani za kuburudika na huvaliwa na kila mfuasi, 1 Wakor. 9:27. Mara nyingi huhitaji kujizuia.
- C. Kunataka "saburi," 10:35-36; 1 Wakor. 15:58; hata kama mtu anaweza akawa "shutumu la hadhara" - "twezo," 10:32-34.

II. Kutia Nguvu Kwa Nguvu Katika Kukimbia Mbio: Shahidi Anayeshuhudia Ushindi, 11.

- A. Mfano wa kushindwa: kutokuamini na kuanguka, ilikuwa "kwa wote pamoja." Waebr. 3; lakini mifano ya ushindi wa wenyewe kuamini, waliokuwa waaminifu ulikuwa sasa kama ni kila mmoja binafsi, Sura 11.
- B. Nuhu --- 11:7 Hapa ni waminifu mbele za fidhuli. Fikiria safina: kipimo chake; wakati uliohusika katika kuijenga; ahadi ya gharika ambayo haijawahi kutokea hapo awali! Bila shaka fidhuli kuu, lakini hatimaye ushindi kwa njia ya imani.
- C. Ibrahim, 11: 8-10. Imani mbele ya jaribio kali, kuacha maskani, kuishi katika mahema. Kiasi cha muda katika kutimiza ahadi, dhabihu ya Isaka. Hata hivyo imani ilivishinda vyote!
- D. Hawa na wengine wengi hushuhudia kuwa mbio zinaweza kumalizwa!

III. Malakwa Ya Lazima Kuhakikisha Ushindi: Kuweka Kando Kila Mzigo Mzito Na Dhambi Ille Itizingayo Kwa Upesi, 12:1.

- A. "Kila mzigo mzito," walikuwa wakijaribu kubebe vipingamizi vingi mno. Mara nyingine ni kufanya kaii zaidi; hakuna muda wa kanisa wala Mungu; mara nyingine ni kununua zaidi; hakuna pesa kwa ajili ya Mungu; mke mbaya,

tabia, mume, rafiki na wote wazizua zo mbio zako. Viondoe! 2. "Dhambi ituzingayo kwa upesi," kila mkristo lazima atoe dhambi yake mpaka hapa: hasira, ghadhabu, uovu, choyo, uasherati; msemo mwovu; ulevi, ni wewe tu na Mungu kuifahamu yako! londoe au uangamie!

IV. Mede Ya Mwisho Mbele: "Tukimtazama Yesu Mwenye Kuanzisha Na Mwenye Kutimiza Imani Yetu," 12:2.

- A. Kama Petro, mkristo mara nyingi huangalia upepo na mawimbi, asimwone Yesu, Math. 14:29-30.
- B. Kufaulu, mkristo lazima awe na nia ya Yesu, kusudi lake moja na mfano wake uwe wetu, Wafil. 2:5-8.
- C. Ni ufahamisho wa namna gani kati ya mashindano yake ya mbio na yetu! Mateso Yake, aibu yake na yetu, Lk. 22: 39-46. Wengine wetu wamelala! Wengine wanacheza katika mashindano, na wengine hawaajaanza hata kidogo!
- D. Ushindi wa mwisho umehakikishwa, 12:4.

Mwisho: Akisha uvumilia msalaba (kumaliza mashindano Yake), na kuidharau aibu aliketi katika Mkono wa kuume wa Mwenye enzi Juu, Utukufu huu amewaaahidia wote wanaomfuata Yeye. Pasipo mateso asingeyama liza mashindano yake, nasi pia vivyo hatuwezi!

Yaoime mashindano yako, mateso, aibu yako na ya Bwana, yako na yangu hupunguka! Mbingu ndiyo taji, waaminifu ndiyo hali, mateso na kujikana ndiyo njia, kwa hiyo uwe na nguvu ndani yake na usizimie! Mungu na atusaidie!

MATATIZO YA KURUDI

Waebr. 12:1-13

Azimio: "Yeye ambaye Bwana Ampenda Humrudi."

Shabaha: Kuonyesha namna mba1i mbali za kuyarudi maisha ya mkristo na uthamani wake.

Dibaji: Moja la matatizo Iisilofahamika 1a kumkabili mkristo ni lile la kuteswa, hasa tatizo la kuteswa kwa ajili ya Kristo unapotenda merna. Maswali yasiyo na hesabu huulizwa:

Je, Mungu huleta mateso? Kama Yeye ni mwema na mwenye nguvu zote, kwa nini asiyazuie kwa ajili ya watoto Wake? Wasio na Mungu humalizia kusema kuwa hata Mungu hana nguvu za kutosha, au kama anazo, si mwema kwa kutosha au sivyo angeweza. Tamati hizi hazitoshe1ezi ambayo mkristo anayafahamu kuhusu Mungu.

Katika somo moja tu sehemu ya juu ya tatizo yaweza ku· guswa, lakini twatumaini kuwa tunaweza kumsaidia *mtu mwaminifu* anayetafuta ukwe1i.

I. Mashindano Ya Mbio Za Mkristo Zinahusu Mateso, 12:1-4.

- A. "Wingu la mashahidi" - ndio hao ambao wamehesabiwa moja moja katika sura ya 11. Wote waliteswa ili kushinda katika kukimbia, kwa hiyo, walishuhudia kuwa tunaweza kushinda mashindano mradi tu tumeyagharamia! Si rahisi - wala yale yao hayakuwa rahisi!
- B. "Na tuweke kando -- mizigo - dhambi." Miano kutokana na kukimbia, weka kando kila kitu kinachokuzuia; kiondoe kinacho kurudisha nyuma! Hapo tu ndipo waweza kukimbia na kufaulu!
- C. "Tukintazama Yesu" - macho yako yawe juu ya yule aliye mbele yako. Yesu hatakupoteza. Aliyamaliza mashindano yake na mwenye kumtimizia kila mmoja wetu. Msaada na nguvu zetu, Wafil. 4: 13.
- D. "Mtafakarini sana Yeye" - alijaribiwa katika mambo yote, aliteswa kiasi ambacho hatutaweza, Waebr. 2:17-18; 4:14-15; 5:8-9.
- F. "Hamjafanya vita - damu - mkishindana na dhambi," mfano wake ni mkuu mno mashindano yetu ni rahisi katika kulinganisha. Endelea!

II. "Ambaye Bwana Ampenda Humrudi," 12:5-6.

- A. Swali linakuja: Kurudi huku ni kimwili au kiroho? Je, kurudi huku ni kuadhibu au kumidhamisha?
- B. Hatuamini kuwa Mungu huleta adhabu ya kimwili katika maisha ya mtu.
 1. Mungu alipoiumba nchi na mtu, alisema ni"nzuri."
 2. Mtu alikosa na daima hugcuza mpango wa Mungu. Mateso yote na mashaka ni matokeo ya dhambi za mtu na mageuzo. Tofauti kubwa katika matokeo ya dhambi kuliko adhabu ya dhambi. Sasa matokeo, baadaye adhabu.

3. Sheria ni hii: "Upandacho - unavuna," Wagal. 6:7 -8. Ni bora kwa mtu kuteswa sasa, ili roho yake imtafute Mungu.
4. Yesu alifundisha kuwa watu huteswa sasa, si kama ndio adhabu ya dhambi, Lk. 13:1-5; Lk. 3:11, 16, (Shetani alimfunga - hakuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake). Tena, mtu aliyezaliwa kipofu, Yoh. 9: 1-3. Hapa Yesu anaonyesha sababu za mateso. Na Waebr. 12 inafanya vivyo.
5. Mwiba wa Paulo katika mwili "mjjumbe wa shetani," 2 Wakor. 12: 7-10. Hakuteswa kwa adhabu ya dhambi.
6. Yesu haadhibu sasa, bali anaokoa, Yoh. 3:17-18.
7. Adhabu ya dhambi itakuja wakati wa kuja kwake Kristo, 2 Wathes. 1:7-10; tunateswa na matokeo ya dhambi sasa, lakini adhabu ya dhambi zetu baadaye wakati wa kuja mara ya pili.

C. Kuteswa na kurudi vinafanya kazi ya utakaso wa roho.

1. Kurudi: fafanuzi, "lo lote ambalo limo katika mtu mzima pia huchimbua roho, hasa kwa kusawazisha makosa na kuzuia tamaa, yaani maonyo yaliyo na shabaha ya kuzidisha wema." Thayer, Waer. 12:5,7.
2. Nidhamu: elimu ya roho ya mwanafunzi; kurudi, kutakasa, kuitakasa roho.
3. Mungu anataka waminifu hata kama itakuwa na gharama gani. Kwa hiyo, kwa njia ya kurudi kila mmoja anatakasika na ulimwengu.
4. Kristo alikamilika katika mateso, Waer. 5:8-9. Kisha mateso yenye, si mapenzi ya Mungu, ila tu, ni matokeo ya mapigano na dhambi, ambayo kwayo tunatimilika. Kwa hiyo, tunafanya mapenzi ya Mungu kugongana na dhambi, kama hatulegei, basi tumenidhamishwa na kwayo tumetakaswa.

III. Tabia Yetu Iweje Na Tunda La Kurudi?

A. Tabia yetu:

1. "Usiyadharau" - ni muhimu katika kuufikia utu uzima wetu kiroho, Yak. 1:2-5.
2. "Wala usizimie moyo ukekemewa naye" - usiache bila kujali kukasirisha.
3. "Kwa hiyo inyosheni mikono" ya kazeni magoti, 12:12-13.

B. Matunda yake:

1. "Tuushiriki utakatifu wake," 12:10. Hapa utakaso unaonekana wazi.
2. "Matunda ya haki," 12: 11. fn. Wafil. 1:11. "Matendo ya wema."

Mwisho: Tatizo hasa la kurudi sio "kwanini" watu wanateswa. Ila tabia yetu iweje juu yake, na zaidi ya hapo, tukufanyie kazi gani. Haya ndio maswali makuu. Mara nyingi kurudi kunachukiza na kufarakisha lakini huku sio kutaka kwa Mungu katika jambo hili. Kila kitu katika maisha haya kimewekwa kwa kufanya roho zetu ziwe bora, fn. War. 8: 28. Mara nyingi ni vigumu kuona au kukubali ila Mungu anatungojea ili tujizoeze nako.

Na tumtukuze Baba wa roho zetu, tukitambua kuwa anajua wanavyotaka, na tuwe na utu mwema na hekima kumwomba Yeye kutusaidia kuelewa na kuitikia itupasavyo.

SINAI AU SAYUNI – UPI?

Waibr. 12:18-31

Azimio: Mungu amekwisha anzisha Ufalme mpya, ambao unachukua nafasi ya Ufalme uliosimamiwa na Sinai.

Shabaha: Kufananisha Ufalme wa kale na mpya na kuonyesha ukuu wa ule mpya.

Dibaji: Mara nyingi mwandishi wa Waibrania amefananisha agano la kale na mpya. Na kila wakati amehakikisha ukuu wa lipya katika kila jambo: Kristo ni mkuu kuliko malaika, Musa na Haruni. Urithi mpya, agano, dhabihu, na ahadi ni kuu kuHko zile za kale. Uhalifu au kuLikana mpya kunasababisha adhabu kubwa zaidi kuLikido ya ile la kale.

Sasa anafanya hoja ya mwisho ufananisho wa Mlima Sinai na vitu vinavyouhusu na Mlima Sayuni na vitu vinavyouhusu. Hili Hna tulazimisha kukata shauri: Utakuwa ni upi? Utauchagua upi?

I. Milima Miwili: Mlima Sinai Na Mlima Sayuni, 12:18-24.

A. Mlima Sinai, 12:18-21.

1. "Uwezao kuguswa," kimwili.
2. "Moto, mweusi na wenyе giza," wa kutisha kwa mambo yake.
3. "Musa alisema, Nimeshikwa na hofu na kutetemeka," hofu inayotia upuzio katika matokeo yake, Taz. pia Kuto. 19; Kumbu. 9:19.

B. Mlima Sayuni, 12:22-24.

1. "Mji wa Mungu aliye hai," wa kiroho, Yerusalemu wa mbinguni, malaika, kanisa la mzaliwa wa kwanza, Mungu mwamuzi, roho za watu wenyе haki, Yesu, agano mpya, damu inenayo."
2. Mzuri katika kuonekana kwake, upendo, Yoh. 3:16; War. 5: 6-8.
3. "Ujasiri" kumjua Mungu, Waibr. 4: 16, kwani Mungu hutusikia, 13:5-6.

C. Yote miwili inasimamia ule wa kitambo na wa milele, mmoja "ulitatemeshwa," mwingine hauwezi kutetemeshwa."

II. Falme Mbili: Wa Kale Na Mpya.

A. Wa kwanza ambao ulipita.

1. Ule ulioanzishwa Sinai, hata hivyo ni ufalme wa kimwili kwa vizazi vya Ibrahimu wa kimwili, hata hivyo ultakiwa kuwa Ufalme wa makuhani na taifa takatifu kwa Yehova, Kut. 19: 5-6.
2. Chini ya uongozi wa Yehova waliipata nehi ya Kanani, kwa hiyo, ahadi ya nchi ya Mungu kwa Ibrahimu Hitimizwa, Yosh. 21 :43-45. Kwa hiyo, hakuna kilicho bakia cha kutimizwa leo!
3. Lakini, kwa sababu ya dnambi zao, iliwabidi kuangamizwa kama taifa, hata hivyo si kama watu, Yer. 19:10.11, yaani walitetemeshwa, kufukuzwa katika nchi, walikataliwa na Yehova, Hosea 4:6: Zek. 11:7-

14; Hagai 2:6. Mungu alifanya jambo hili hilo kwa kulitumia jesbi la Kirumi kuliharibu taifa la Kiyahudi mnamo mwaka 70 B. K.

B. Upya "ambao hauwezi kutetemeshwa."

1. Ufalme huu ulibashiriwa na manabii: Isa. 2: 1-4 (Fafanua - wakati, mahali, mahali pote, namna yake; Dan. 2:44 (Fafanua: wakati, namna yake); Dan. 7:13-14; (Fafanua: siku za kale, ufalme, mataifa, milele, namna yake,)).
2. Vyote vilitimizwwa: Lk. 19: 11-27 (Fafanua nchi ya mbali kuupokea ufalme, kurejea, kuamriwa na kutuzwa watumwa, adhibiwa na kuangamiza maadui, mahali pote, Math. 28:18-20; namna yake, Waef. 2:14-17; Waebr. 12:14; milele, Waebr. 12:28. Mwishoe ulikabidhiwa kwa Mungu, 1 Wakor. 15:22-26.

III. Je, Sisi Kama Kila Mmoja Binafsi, "Tunaupokea Namna Gani Ufalme Huu Wa Milele Usio Tetemeshwa?

- A. "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili," Yoh. 3:1-7.
 1. "Kwa maji," Tit. 3: 5; Waef. 5:26-27; Math. 28:18-20.
 2. "Kwa Roho," War. 8: 14; Mdo. 2: 1-4; 2: 38.
- B. "Hamna budi kuabudu katika roho na kweli," Yoh. 4: 24.
 1. Tukiongozwa na mamlaka ya Kristo, Wakol. 3:17.
 2. Tumetakaswa na kweli, Yoh. 8:32; 17:17; War. 10:17.
- C. "Hamna budi kuwa watakatifu kama alivyo mtakatifu," 1 Pet. 1:15.
 1. Jinsi Mungu alivyo ndicho kipimo chetu, Math. 5:48; 1 Pet. 1:15; Yoh. 3:3.
 2. "Hatuna budi kuzionyesha fadhili zake, 1 Pet. 2:9-10.

Mwisho: Sasa utauchagua upi? Sinai au Sayuni? Wa kimwili au wa kiroho, wa kitambo au wa milele? Uchaguzi ni wako na ni wewe peke yako unaweza kuufanya, ila kumbuka 12:25-29.

WAJIBU WA MKRISTO

Waibr. 13:1-17

Azimio: Kwa sababu tu wakristo, waliyo milki ya Krista, tunao wajibu kwa watu na dini ambaao ni lazima kuutimiza.

Shabaha: Kuonyesha wajibu fulani kwa watu na dini ambaao hatuna budi kuutimiza kama wakristo.

Dibaji: Thibitisho halisi la ukristo kwa ulmwengu ni maisha ya mtoto wa Mungu. Ni muhimu sana jinsi tunavyoishi, kwani maisha yetu huonyesha zaidi kwa wazi kabisa imani yetu, kuliko hoja zetu kuhusu jambo tunaloliamini!

Biblia mara nyingi lamsihi mkristo kwamba nuru yake iangaze, Math. 5:13-14, kuyawezesha maisha yako kuleta utukufu kwa Mungu, 1 Pet. 2:11-12.

Si kwamba tu wakristo wa Kiebrania walihitajika kujifunza ukuu wa kila kitu kuhusu agano mpya, lakini pia walitakwa kutimiza mambo kadhaa ya watu na dini ambayo pia yamhusu kila mmoja wetu kama wakristo.

I. Wajibu Kwa Watu Ambao Ni Lazima Mkristo Auheshimu.

A. "Upendano wa ndugu na udumu," 13:1.

1. Amri mpya ya Yesu ilikuwa ni nishani ya wanafunzi, "upendano wa ndugu," Yoh. 13:34-35.
2. Uwe ni upendano wororo; upendo wa usafi na furaha, 1 Pet. 1:22.
3. Lazima udhihirike *katika* "kuonyesha kuwafadhili wageni," 13:2 fn. War. 12:13; 1 Pet. 4:9; 1 Tim. 3:2; Hili litakuwa muhimu siku ya Hukumu, Math. 25:35.
4. Lazima udhihirike katika "kuwakumbuka waliofungwa na wanaodhulumiwa," 13:3. Hii ndiyo huruma hasa na ushirikiano wa wakristo, Mat. 25:26; War. 12:15; Wagal. 6:2.

B. "Ndoa na iheshimiwe na watu wote," 13:4. Onyo juu ya kutokuwa safi.

1. Ndoa ya toka kwa Mungu, Mwa. 2:18; 2:24. Hapo wote lazima waiheshimu.
2. Useja na aeshiki isiyofaa *imekuwa ni* kaimu wa Shetani katika vizazi, 1 Tim. 4:1-3
3. "Mungu atawahukumu," Ufu. 2:20-23.

C. "Msiwe na tabia ya kupenda fedha," 13:5.

1. Upendo wa fedha uliwatambulisa Wayahudi tangu *siku za* Yakobo. Kutarnani kumekuwa *katika* kundi lilo hilo pamoja na uchafu, 1 Wakor. 5:11; 6:9-10; Waef. 5:5; Wako1. 3:5; 2 Pet. 2:14.
2. "Kuridhika na ulivyo navyo," Uradhi uwe ndio lengo la kila mkristo, 1 Tim. 6:6-8; ambaao Paulo alijifunza, Wafil. 4:11-12.

D. "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa," ahadi ya rehema ya Mungu imfanye kila mmoja asiogope mambo yaliyopo au ya baadaye, akiongozwa katika kuridhika katika kila hali.

II. Wajibu Wa Dini Ambao Ni Lazima Kila Mkristo Auheshimu.

A. Dhabihu na ibada zifanywe kwa njia ya Kristo, 13:15-16.

1. "Na tumpe Mungu dhabihu ya sita," kwa sababu ya dhabihu ya Kristo sasa tunayo madhababu ambapo sisi tunayo haki ya kula, "tunda la midomo," sifa inayodumu, ya kila siku! Wafil. 4:4-6.
2. "Na tutende mema na kushirikiana," msaada wa kudumu kwa hao wanaohitaji, Wagal. 6:10; 1 Tim. 6:17-19.

B. "Watiini wenye kuwaongoza," 13:17.

1. Wakristo lazima wa watii wazee wa kusanyiko, fn. 13:7.
2. Wakristo lazima "waiige imani yao," 13:7. Wao ni kielelezo chetu.
3. "Wao, "wazee" watiitoa hesabu," 13:17.
4. "Wanakesha kwa ajili ya roho zenu," ole wao wazee wasiofanya hivyo!
5. "Watatoa hesabu," kwa Mungu! Wazee wana wajibu juu ya kusanyiko, 1 Pet. 5:1-4.

C. "Msichukuliwe na mafundisho ya namna nyingine nyingine na ya kigeni," 13:9.

1. Msisite na kuikataa kweli, 2:1-3.
2. Kweli uifanyie kazi "pambanua mema na mabaya," 5:11-14.

Mwisho.: Hekima ya Mungu ni wazi kwa wote wanaotaka kuona. Hakuna mtu aliye kisiwa! Ukristo haukumaanishwa kuwa katika utupu. Tutakutana na wajibu na Mungu anatuhakikishia ushindi ndaniya Kristo. Je, utamkubali Kristo huyu, mwokozi wako, na kuyaanza mashindano ya Mkristo!

KRISTO ASIYEBADILIK

Waeb. 13:7-9

Azimio: "Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele."

Shabaha: Kuonyesha imani, Kristo na injili isiyobadilika.

Dibaji: Mwanadamu kila siku anataka kubadili kila kitu, hasa kilicho chema, cha kweli na kisafi. Wanadamu daima wan atafuta kuyabadili mafundisho ya Kristo, kwa hiyo, Roho Mtakatifu ametuonyakuwa Kristo habadiliki!

Hoja iliyofanyika na mtume sasa imetimilika. Ameonyesha mara kwa mara ukuu wa njia yote ya ukristo kwa ile ya Musa na sheria, na ameonyesha jinsi ile ya awali ilivyoonyesha kwa hii ya sasa. Hoja yake ya mwisho ni kwa ajili ya waminifu katika msingi wa kutokubadilika kwa Kristo.

Mawazo matatu yameingizwa: (1) Imani ya waalimu wao wa awali, ambao imani yao ilikubaliwa kwa Mungu na inafaa kuiiga; (2) Kutokubadilika kwa Kristo ambako ndio msingi wa imani inayokubaliwa; upuzi wa kusikiliza mafundisho mageni, kwani imani ya kweli inatokana na fundisho linalotosheleza. Haya tunayatafakari.

I. Imani Ya Kuiga Ni Imani He Isiyo badilika, 13:7.

- A. "Wakumbukeni wa!e waliokuwa wakiwaongoza," si wale mashujaa wa sura ya 11 tu, bali waalimu wao katika injili, Stefano, Yakobo na Petro, Wayahudi wote waliwahubiria wakristo wa Kiebrania.
- B. "Waliowaambia neno la Mungu," si mafunzo tu, bali, mausia ya Mungu," 1 Pet. 4:11. "Ukweli ulivyo ndani ya Yesu," 2 Tim. 4:1-2. Haibadiliki katika hali zote, ni injili moja au hakuna injili! Wagal. 1:6-9.
- C. "Kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao," kuondoka kwao, mwisho labda kifo chao, Stefano, Yakobo, (Mdo. 7; 12; nk.) "mwaminifu hadi kufa," Ufu. 2:10.
- D. "Igeni imani yao," waliishi na kufa kwa utukufu wa Mungu, wafuatensi wao! Kuwa imara kwao, Waef. 4:5; Yuda 3; Ufu. 2:10.

II. Yesu Kristo - Mwanzilishi Wa Imani Isiyobadilika, Ni Kristo Asiyebadilika.

- A. Yesu Kristo ni yeye yule," habadiliki. Kila siku namna yake ni Mungu, Yoh. 10:20, sasa na daima, Yoh. 17 :4-5.
- B. Tabia yake "haibadiliki" - hushikilia tabia ile ile daima kwa Mungu, kwa mtu, kwa dhambi. Habadiliki; hana kigeugeu, wala kusita sita. Kwa hiyo kwa njia yake, na kwa njia Yake tu, mtu aweza kumfikia Mungu, Yoh. 14: 6; njia Yake, Math. 7:13-14.
- C. Kazi yake ya ukombozi "haibadiliki." Mtu ni mwenye dhambi mpaka sasa na amekuwa hivyo siku zote, kwa hiyo anahitaji mwokozi, anahitaji damu, Waeb.

- 9:22; 9:13-14; Imani, Waebr. 11:6; kuifikia damu Waebr. 10:19-20; Waminifu, Waebr. 3:14; 12:1-3; 12:14.
- D. Kazi yake au upatanisho na usu1uhishi "haibadiliki." 2 Yoh. 2: 1-2; Waebr. 4: 15-16; 7:25.
- E. Kazi yake ya Msaidizi wa watu Wake na mahitaji yao "HaibadiIiki." Math. 28:20; Waebr. 13:6. Angali anakesha na kusikiliza kilio cha roho zinazohangaika na kuhuzunishwa!

III. Kutokana Na Kristo Asiyebadilika lmekabidhiwa Huduma Isiyobadilika:" Moyo Ufanywe Imara Kwa Neema," 13:9.

- A. "Msichukuliwe na mafundisho ya kigeni." Angalia, "mafundisho ya mashetani" 1 Tim. 4:2; "mafundisho ya wanadamu" Math. 15:8; Wakol. 2:22; Lakini kila siku ni "fundisho" katika umoja, likiwa ni fundisho la Mungu, Kristo au Mitume! Lao ni "njema, la maana" nk.
- B. "Moyo ufanywe imara kwa neema." Neema na kweli vilikuja kwa njia ya Kristo, Yoh. 1: 19; kweli hii itaidumisha neema yote, Mdo. 20:32; neno na kweli ambayo haibadiliki na inadumu vizazi vyote, Math. 24:35; 1 Pet. 1:24-25. Kufanya imara huku miyo yetu ni kwa njia ya Kristo, Tit. 2:11-14; Waef. 4:20-24.

Mwisho: Mungu anawahitaji wanaume na wan awake wenye imani ya namna hiyo! Watu bado wangali wanamhitaji Kristo asiyebadilika uyo huyo. Wewe na neno moja lisilobadilika na ni sisi tu katika ulimwengu amba Mungu amewakabidhi. Kazi yetu ni kubwa, sai letu la kuogofya, lakini Kristo ni mkubwa sana! Sifa kwa Mungu.